UKURASA WA 2

**Mnyika** atangaza siku 10 na masharti uchaguzi CHADEMA



UKURASA WA 3

**Tarehe** kumpata mrithi wa Kinana CCM yatajwa

UKURASA WA 5

**Dereva** bajaji aliyetangaza kuuza mtoto atiwa mbaroni

**GUARDIOLA AMPA ONYO GREALISH** UK. 22


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Januari 8, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581915

Nipashe digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com

Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii

www.ippmedia.com


MAUAJI KATIBU CCM

# Ulinzi mkali kortini wakisomewa upya mashtaka dhidi yao

• **Makada**, ndugu wafurika kortini, washtakiwa wengine 'wawapa tano' waandishi... *Uk. 3*



Watuhumiwa wa mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilolo, Christina Kibiki, wakifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Gambo aja na hoja zake kumjibu RC Makonda

UKURASA 18

## Samia atoa miezi mitatu waliokodi visiwa Zanzibar wakavitelekeza, wanyang'anywe

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan na Mwekezaji Andrea Azzola wakivuta kitambaa kuashiria ufunguzi wa hoteli iliyoko Kisiwa cha Bawe, Zanzibar jana, wakati wa shamrashamra za kuelekea miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **YANGA NA HESABU KALI KUIVAA AL HILAL** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Samia atoa miezi mitatu waliokodishwa visiwa wakavitelekeza, kunyang'anywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wametoa miezi mitatu kwa waliokodishiwa visiwa kufanya uwekezaji vinginevyo watapewa wengine.

Viongozi hao wamesema kuna wawekezaji wengine wanaohitaji visiwa hivyo kwa ajili ya kuweka miradi ya kiuchumi kwa maendeleo ya Zanzibar na taifa kwa ujumla.

Wamesema visiwa hivyo vina faida kubwa katika uwekezaji na kila jambo jipya lina mambo yake kwa sababu serikali ya Zanzibar ilipotangaza kuwekeza katika visiwa, baadhi ya watu walikuwa wakali.

Rais Samia na Dk. Mwinyi waliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa hoteli ya Bawe katika Kisiwa cha Bawe ambacho ni moja ya visiwa 15 vilivyokodishwa na serikali ya Zanzibar kwa ajili ya uwekezaji.

Dk. Mwinyi alisema wawekezaji waliokodishwa visiwa na hadi sasa hawajafanya uwekezaji wowote, baada ya miezi mitatu, visiwa hivyo vitarejeshwa serikalini ili kupewa wengine wenye uwezo.

Rais Samia alisema hivi sasa kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika hakuna anaejuta kwa sababu unakuza pato la taifa.

Alisema amefarajika na uwekezaji wa visiwa vidogo na kuwapongeza wawekezaji pamoja na Mamlaka ya Kukuza Vitegauchumi Zanzibar (ZIPA) kusimamia kazi hiyo visiwani hapa.

Samia alisema hiyo ni ishara tosha wawekezaji wanaridhika na kufanya uwekezaji ikizingatiwa kuwa sheria za uwekezaji zimefanyiwa marekebisho.

Pia alisema katika uwekezaji huo, gharama zilizotumika ni Dola za Marekani milioni 42 ambazo si ndogo na kuna uwekezaji mkubwa umefanywa ukiwamo kutengeneza umeme wa jua na kubadilisha maji ya chumvi kuwa maji safi kwa matumizi ya hoteli hiyo.

Alisema Zanzibar ilikua na visiwa ambavyo vingekuza uchumi lakini uchumi ulikaliwa, hivyo kutumiwa na wavuvi pekee.

Eneo hilo la kisiwa cha Bawe, limeleta manufaa makubwa ikiwamo ajira 400 kwa vijana na wawekezaji watalipa kodi kwa serikali na kupata mapato, hivyo kukuza jina la Zanzibar.

Alisema mbali na maeneo mazuri ya uwekezaji, serikali imedhamiria kufanya mambo mengi ikiwamo uwekezaji katika bandari zikiwamo ya makontena ya Malindi, ya mizigo ya Fumba, Mpigaduri, Mkoani Pemba na bandari ya kushusha mafuta na gesi Mangapwani.

Kwa mujibu wa Rais Samia, hayo yote yatakuza uchumi wa buluu na kupata maendeleo makubwa.

Alisema katika jitihada za kuifungua Pemba kiuchumi, serikali inatarajia kujenga bandari kubwa ya abiria na mizigo Wete Pemba pamoja na bandari ya Kizimkazi, Kusini Unguja.

Uwekezaji huo, alisema utaimarika na juhudi za serikali kuimarisha viwanja vya ndege na wasafiri watavutiwa na huduma, hivyo aliwataka watendaji katika viwanja vya ndege kuongeza jitihada katika kutoa huduma.

"Uwekezaji kufika visiwa ni jambo jipya kuendelea kuelimisha wananchi ili lisilete shida katika mahusiano," alisema na kuwataka watumiaji wa visiwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali na wawekezaji ili kuleta matokeo makubwa kwa maendeleo ya uchumi.

Rais Mwinyi kwa upande wake, alisema Rais Samia amekuwa msaada mkubwa kwa serikali ya Zanzibar katika mambo mbalimbali.

Dk. Mwinyi alimpongeza mwekezaji wa kisiwa cha Bawe kuwa amefanya kazi nzuri kwa kuwa uwekezaji aliofanya ni wa kiwango cha kimataifa.

Alisema wawekezaji wameendelea kuwasaidia wavuvi kwa ajili ya shughuli zao katika eneo hilo na samaki wanaowapata huwauza katika hoteli zilizomo kisiwani humo.

Rais Dk. Mwinyi alizitaja faida za uwekezaji kuwa ni pamoja na ajira na kuwataka Wazanzibari kusoma ili kuhudumu katika ajira kwenye sekta ya utalii. Faida nyingine ni kukua kwa masoko au bidhaa na kuongezeka kwa watalii.

Waziri Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif, alisema uwekezaji huo ni historia ya kipekee kwa sababu mengi yaliyopita kupitia visiwa hivyo, faida yake imeonekana.

Mkurugenzi Mkuu wa ZIPA, Saleh Saad, alisema mabadiliko na ukuaji na uwekezaji katika visiwa vya Zanzibar ni makubwa.

Uzinduzi wa mradi huo wa hoteli ya Bawe ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# Mnyika atangaza wiki mbili na masharti uchaguzi CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimetangaza wiki mbili za kujifungia kwenye vikao vya kuwapata viongozi wa nafasi mbalimbali ndani ya chama hicho katika uchaguzi utakaofanyika Januari 22 mwaka huu.

Vilevile, kimetoa tahadhari kwa wanachama, wagombea na mawakala au wapambe wao, kuzingatia Katiba, miongozo, kanuni, taratibu na itifaki ya chama hicho katika mchakato mzima wa uchaguzi na kwamba ipo hatari ya wagombea kuondolewa katika kinyang`anyiro endapo itathibitika kukiuka hayo.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika ndiye alitangaza hayo jana wakati anazungumza na waandishi wa habari kwenye Makao Makuu ya chama hicho mkoani Dar es Salaam.

Alisema vikao hivyo ni vya usaili na uteuzi wa wagombea pamoja na uchaguzi wenyewe.

"Kwa kweli tutakuwa na vikao vya chama mfululizo, ni 'marathon' ya vikao vya kama wiki mbili hivi, vitahusisha usaili, uteuzi wa wagombea na baada ya kukamilika kwa hatua hiyo, kutafuata hatua ya uchaguzi wenyewe," alisema.



Alisisitiza kwamba kuelekea katika uchaguzi huo, wanachama, wagombea pamoja na mawakala wao, wanatakiwa kuzingatia Katiba, kanuni, miongozo, taratibu na itifaki ya chama hicho.

"Wakati ninatoa tangazo la uchaguzi, nilitoa wito kwa wagombea, wanachama na mawakala wa wagombea, kuzingatia Katiba, kanuni, maadili na itifaki ya chama katika mchakato mzima wa uchaguzi na mahususi nilitaka wazingatie miongozo miwili muhimu ya chama katika kipindi hiki cha uchaguzi ambayo ni ule unaohusiana na taratibu za kuendesha kampeni ya uchaguzi ndani ya chama na ya rushwa yote ya mwaka 2012.

"Hata hivyo, katika kipindi hiki cha uchukuaji na urudishaji fomu, kumejitokeza vitendo ambavyo vinaashiria kuvunjwa kwa miongozo hii na baadhi ya wanachama au wagombea, kuna tuhuma za namna mbalimbali za namna hiyo," alisema Mnyika.

Aliwataka kusoma masharti ya msingi yaliyomo katika miongozo hiyo na kwamba iwapo kuna kiongozi, mwanachama au mgombea atakayeikiuka, malalamiko yawasilishwe katika ofisi yake ili hatua zichukuliwe kudhibiti hali hiyo.

"Kwa masharti yanayohusu taratibu za kampeni, CHADEMA ni chama kinachoamini katika demokrasia, usawa na maadili ya kweli na kwa kuwa maadili ya chama ndiyo yanayoainisha sifa za uongozi wa chama.

"Sifa hizo ambazo ni pamoja na nidhamu, utii, uwajibikaji na dhamira ya wanachama, viongozi na chama katika ngazi mbalimbali kwa muundo wa chama na jinsi ya kuwapata na kuwapima viongozi.

"Hivyo basi, mwongozo huu unalenga kuhakikisha kuwa kampeni zinafanyika kwa uwazi, haki na kwa kufuata misingi ya demokrasia," alisema Mnyika.

**YASIYOTAKIWA**

Mnyika alisema wagombea au mawakala wao wakati wa kampeni, wanatakiwa wafuate taratibu kwa kutofanya kampeni hizo kabla ya muda wake kutangazwa na mamlaka husika ndani ya chama hicho.

Pili, mgombea au wakala wake, kama ilivyosisitizwa na Mnyika, hatoruhusiwa kufanya kampeni chafu kwa kumkashifu mgombea mwenzake kwa kusambaza nyaraka, vipeperushi au taarifa kwa njia ya mitandao ya kijamii zisizohusiana na wasifu wake.

Tatu, Mnyika alisema ni marufuku kusambaza taarifa kwa njia yoyote ile zenye lengo la kukashfu mgombea au kiongozi wa chama na sharti la nne ni marufuku kwa mgombea au wakala wake kufanya kampeni kwa kuhusisha ukanda, udini ukabila au ubaguzi wa aina yoyote ile.

"Tano, mgombea au wakala wake, anatakiwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika mwongozo dhidi ya rushwa. Sita, mgombea au wakala wake atatakiwa kuwa na sifa kama zilivyoainishwa na Katiba na kanuni za chama hicho.

"Saba, mgombea au mwakilishi wake hatoruhusiwa kufanya kampeni kwa kujinasibu na kiongozi yeyote wa kitaifa, wilaya au kiongozi yeyote wa kuchaguliwa iwe kwa mazuri au kwa mabaya," alisema.

Mnyika alitaja adhabu za ukiukaji mwongozo na kanuzi hizo kuwa ni pamoja na kupewa onyo, onyo kali kwa kosa la pili na kwa kosa la tatu ataondolewa katika mchakato wa uchaguzi endapo itadhibitika kuwa mgombea kufanya makosa hayo.

Adhabu ya nne, Mnyika alisema ni kufungiwa kugombea nafasi yoyote ya uongozi ndani ya chama hicho kwa muda utakaotajwa na mamlaka husika usiozidi miaka mitano.

**KUDHIBITI RUSHWA**

Mnyika, akizungumzia mwongozo wa kudhibiti rushwa katika kampeni za chama hicho, alisema mwanachama, kiongozi au wakala wake hawaruhusiwi kutoa fedha kwa njia yoyote ile, vyakula, vinywaji au zawadi nyinginezo kwa wajumbe au wapigakura kwa lengo la kujipatia kura.

Alisema mwongozo huo unakataza kuwasafirisha wajumbe au wapigakura kuhudhuria mkutano au kituo cha kupigia kura kwa ngazi husika kwa ajili ya uchaguzi kwa lengo la kujipatia kura.

Alisema mwongozo huo pia unakataza kutoa ahadi zenye lengo la kuwalipa fadhila wajumbe au wapigakura baada ya kupiga kura kukamilika, kuandaa kikao chochote cha wapigakura kwa lengo la kuwapa fedha, chakula au zawadi zingine bila kuzingatia taratibu za kampeni zilivyoainishwa na kutoa au kushinikiza, kupokea au kushawishi rushwa ya ngono.

Mnyika alisema alisema mwongozo huo pia unakataza kutumia mamlaka ya uongozi kwenye chama kupendelea upande mmoja wa mgombea na kutumia dhamana ya uongozi ili kujinufaisha binafsi kisiasa au kimali wakati wa uchaguzi.

"Mtu yeyote anayetuhumiwa kufanya kosa ndani ya CHADEMA, mwanachama au kiongozi, kabla hajachukuliwa hatua, anatakiwa kuandikiwa tuhuma zake na kupewa nafasi ya kujitetea halafu vikao vya uamuzi vifanye uamuzi kwa mujibu wa mamlaka za kinidhamu za kuchukua hatua husika," alisema Mnyika.

Katibu Mkuu huyo alisema Katiba ya chama hicho imetoa mamlaka kwa kamati ya wazee wastaafu kusimamia uchaguzi huo, akidokeza kuwa "kulikuwa na maneno kwamba labda kura zitakwenda kuhesabiwa kwa kificho na utaratibu mwingine, niwahakikishie kwamba kura zitahesabiwa kwa uwazi palepale ukumbini."

Kuhusu wajumbe wa Kamati Kuu walioonesha mapenzi au upande wao wanaounga mkono, Mnyika alisema hiyo si shida kwa sababu uamuzi unafanywa na kamati nzima.

Jumla ya wagombea 300 wamerejesha fomu ya kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo kuanzia ngazi ya kitaifa hadi mabaraza yake.

Kwa nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, aliwataja wanaogombea kuwa ni Freeman Mbowe, Tundu Lissu na Odero Charles.

Nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara, wanaogombea ni Ezekiel Wenje, John Heche na Mathayo Gekul wakati Makamu Mwenyekiti Zanzibar wagombea ni Said Mzee Said, Said Issa Mohamed, Suleiman Makame Issa na Jafidh Ally Salehe.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# Kombo asifu ushirikiano wa Tanzania na China

**Ye Tianfi na Ning Yi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, amepongeza mafanikio yaliyofikiwa na Baraza la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC).

Akizungumza katika mahojiano na gazeti la China Daily mwishoni mwa wiki, Kombo alisisitiza kuwa ushirikiano baina ya China na Afrika si tu umekuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii Tanzania, bali pia umeleta matokeo chanya kwa bara zima la Afrika.

Akitoa mfano wa kilimo cha soya kwa umuhimu wa maendeleo ya miundombinu kwa ajili ya kilimo cha kisasa, Kombo alisema kimeongeza tija na mauzo ya zao hilo nchini China, hivyo kunahitaji mitambo, maendeleo ya kisasa na uboreshaji wa miundombinu na haya ni maeneo yanayohusiana sana na ushirikiano na China.

"Kwa kushirikiana na China, Tanzania inaweza kuboresha hali ya usafiri na kupunguza gharama za usafirishaji, hivyo kuongeza ushindani wa soko la mazao ya kilimo," alisema Kombo.

Balozi Kombo alizungumzia hatua 10 za ushirikiano zilizotangazwa kwenye mkutano wa FOCAC, ambazo zinashughulikia mahitaji muhimu ya Afrika, kama vile ustawi wa biashara, mnyororo wa viwanda, uunganishaji, kilimo, mambo ya afya, maisha ya watu na maendeleo ya kijani.

Kombo alisisitiza hatua ya ubia kwa maendeleo ya kijani ambayo ni moja ya hatua 10 za ushirikiano ambayo inawakilisha uwezo wa ushirikiano katika maendeleo ya kijani.

Alisema ana imani juu ya mustakabali wa ushirikiano wa maendeleo ya kijani kati ya China na Afrika.

"China inaongoza duniani kwa teknolojia na soko katika sekta ya betri. China na Tanzania zinaweza kufanya ushirikiano wa kina katika mnyororo wa viwanda vya betri ili kutoa fursa zaidi za ajira za ndani na kukuza mabadilishano ya kiufundi," alisema.

Malengo Sita ya Maendeleo ya Kisasa na Hatua Kumi za Ubia zilizotangazwa na FOCAC 2024 zimetoa maarifa muhimu kwa ushirikiano wa Tanzania na China, hasa katika mambo ya mabadiliko ya kilimo na maendeleo ya kijani.

Ushirikiano wa Tanzania na China katika kukuza kilimo cha kisasa unaonesha umuhimu wa ushirikiano katika mnyororo wa viwanda. Kupitia maendeleo ya miundombinu na mitambo ya kilimo, tija na ushindani wa soko unaweza kuimarika.

Katika ushirikiano katika sekta ya betri, uunganishaji wa rasilimali za madini ya Tanzania na teknolojia ya China utakuza maendeleo ya sekta mpya ya nishati ya pande hizi mbili na kuleta fursa za ajira na uboreshaji wa viwanda Tanzania.

# Washtakiwa mauaji kigogo CCM wasomewa upya mashtaka yao

**Na Francis Godwin,** IRINGA

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya mauaji inayowakabili watuhumiwa watano, umewasomea upya shtaka hilo kwa kuwaunganisha watuhumiwa wote watano.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Diwani wa Nyanzwa, Boniphace Katili, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM ) Wilaya ya Kilolo, Hedikosi Kimwaga na wenzao watatu.

Wote kwa pamoja walifikishwa tena mahakamani jana saa 3:47 asubuhi kwa magari mawili; aina ya Landa Cruiser yenye namba za usajili PT 1909 na KM 91 MS -GP yaliyosindikizwa na askari waliobeba silaha mbalimbali na mabomu ya machozi.

Kwa muda wote kabla ya watuhumiwa hao kufikishwa mahakamani, wananchi wakiwamo ndugu wa marehemu, viongozi wa jumuiya za CCM na makada wa vyama mbalimbali na wasio na vyama, walijitokeza kufuatilia kesi hiyo tofauti na siku ya kwanza ambayo walikuwapo ndugu wa watuhumiwa pekee ambao hawakuzidi 10.

Washtakiwa walifikishwa mahakamani huko jana mbele Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Rehema Mayagilo kwa tuhuma za mauaji ya aliyekuwa Katibu wa CCM Wilaya ya Kilolo, Christina Kibiki.

Washtakiwa wote ni Kefa Wales, Silla Kimwaga, Boniphace Katili, Willy Chikweo na Hedikosi Kimwaga.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Sauli Makori alidai mahakamani huko kuwa mshtakiwa namba moja katika kesi hiyo, Wales, alifikishwa mahakamani na kusomewa shtaka hilo pekee yake kabla ya watuhumiwa wengine wanne kusomewa shtaka hilo, hivyo akaomba kusoma upya maelezo ya shtaka kwa watuhumiwa wote watano.

Akisoma upya maelezo ya kesi hiyo ya jinai namba 34404 ya mwaka 2024 ya mauaji, alidai kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Novemba 12, 2024 katika kijiji cha Ugwachanya, wilayani Iringa. Hata hivyo alisema upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Hakimu Rehema alisema watuhumiwa hawapaswi kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo kisha akaiahirisha hadi Januari 21 mwaka huu saa tatu asubuhi itakapotajwa tena.

Baada ya kuahirishwa kwa kesi hiyo, wakati watuhumiwa hao na wengine wakipandishwa kwenye gari kuelekea mahabusu gerezanim, baadhi ya washtakiwa wa kesi zingine walisikika wakipaza sauti kuwapongeza waandishi wa habari kwa kutimiza wajibu wao.

"Kazi nzuri... kazi nzuri waandishi... pigeni kazi..." walisikika baadhi ya washtakiwa hao wakati wakiingizwa katika moja ya magari yaliyotumika jana kuwafikisha mahakamani washtakiwa wa kesi hiyo ya mauaji.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza wakati akifungua mafunzo maalum ya siku tano kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yanayohusu usimamizi wa fedha za umma, yaliyoandaliwa na Wizara ya Fedha kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, yaliyofanyika jijini Arusha jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Tarehe kumpata mrithi wa Kinana CCM yatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAFASI iliyoachwa wazi na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana inatarajiwa kuzibwa wakati wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama hicho uliopangwa kufanyika Januari 18 na 19 mwaka huu jijini Dodoma.

Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo (CCM), Amos Makala alibainisha hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi habari kuhusu maandalizi ya mkutano huo.

"Ajenda ya kwanza kwenye Mkutano Mkuu huu wa Taifa ni kufanya uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara. Kama mnavyojua kuwa nafasi hii ipo wazi baada ya Abdulrahman Kinana kuomba kupumzika. Kwa hiyo Mkutano Mkuu huu tutautumia kujaza nafasi hiyo iliyo wazi.

"Ajenda ya pili itakuwa kupokea kazi za chama katika kipindi cha 2022 hadi 2025. Kwa hiyo mkutano mkuu utapokea kazi za chama zilizofanyika katika kipindi hiki baada ya uchaguzi ndani ya chama 2022 hadi tulipo sasa," alisema.

Makala alisema ajenda ya tatu itakuwa ni kupokea taarifa ya utekelezaji ilani ya uchaguzi kwa kazi zilizofanywa na serikali zote mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na zile zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Kwa hiyo hizo ndizo ajenda tatu lakini pia nimeeleza tarehe ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu. Nitumie nafasi hii kusema kwamba kumekuwa na ubashiri mwingi kwenye vyombo vya habari, unaona vichwa vya habari kwamba CCM ni patashika, wafuatao watajwa kuritihi nafasi ya Kinana.

"Wengine nani wanasema nani kati ya hawa atarithi nafasi ya Kinana, wengine wanakwenda mbali zaidi na kusema kwamba wafuatao wajitokeza kurithi nafasi ya Kinana. Kwa hiyo kila mmoja anaandika anavyotaka," alisema Makala.

Alisema nafasi ya Makamu Mwenyekiti haigombewi wala mtu hajazi fomu, hivyo kusema ni kinyang'anyiro si sahihi.

"Nafasi hi haigombewi wala mtu hajazi fomu kuomba kuchaguliwa, nitakushangaa kwa nafasi ambayo haigombewi na wala hujazi fomu kinyanyang'anyiro hicho kinatoka wapi," alisema.

Makala alisema mrithi wa Kinana atapatikana kutokana na Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa kupendekeza jina ambalo litawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu na hapo ndipo zitapigwa kura za ndiyo na hapana ili kumpata Makamu Mwenyekiti.

"Kwa hiyo wale ambao walikuwa wakibashiri na kupiga ramli sasa muda huo haupo, huo ndiyo utaratibu wa kumpata Makamu Mwenyekiti, unapendekezwa, inawezekana miongoni mwenu tuna Makamu Mwenyekiti wa Bara humuhumu mlipo," alisema.

Alisema kikao cha Kamati Kuu na kile cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa vinatarajiwa kufanyika Januari 16, 2025 ambapo ndipo litapatikana jina hilo kabla ya kupelekwa kwenye Mkutano Mkuu.

Mwenezi huyo alisema maandalizi ya mkutano huo yamekamilika na hivi sasa wanajiandaa kuwapokea wajumbe wa mkutano huo na waalikwa watajulishwa.

Ilitangazwa kuwa Kinana aliandika barua kuomba kustaafu kwenye nafasi hiyo tangu Julai mwaka jana kwa madai ya kutaka kupumzika. Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan aliliridhia ombi hilo.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# HABARI PICHA



Naibu Meneja Mkuu wa The Guardian Ltd, Jackson Paul akimkaribisha Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, kutembelea kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana.



Balozi wa China akisalimiana na Meneja wa Teknolojia ya Habari, Allan Mshana.



Mhariri Mtendaji wa gazeti Nipashe, Beatrice Bandawe, akitambulishwa kwa Balozi wa China nchini, Chen Mingjian.



Balozi wa China akiangalia namna mchakato wa uchapaji wa magazeti unavyofanywa wakati alipotembelea kiwanda cha uchapaji cha The Guardian Ltd Mikocheni jijini Dar es Salaam jana.



Uongozi wa Kampuni ya The Guardian Ltd ukiwa katika mazungumzo na Balozi huyo baada ya kutembelea kampuni hiyo jana.



Naibu Meneja Mkuu, Jackson Paul (katikati) na Mhariri Mtendaji wa gazeti The Guardian, Wallace Mauggo (kushoto), wakipokea zawadi ya Heri ya Mwaka Mpya kutoka kwa Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

HABARI KITAIFA

# Wapandishwa kizimbani kwa mashtaka 68 kusababishia TRA hasara ya bilioni 2.1/-

Na Grace Gurisha

VIJANA sita wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam na kusomewa mashtaka 68 yakiwamo ya kufanya udanganyifu kwenye mashine za kielektroniki (EFD), hivyo kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. bilioni 2.1.

Vijana hao ni mfanyabiashara Stanslaus Mushi (27) mkazi wa Malamba Mawili,

Nemence Mushi (29), Rose Nanga (33), Mhasibu wa Soko Mkazi wa Kimara B,

Hussein Mlezi (37), Fundi wa Kompyuta Mkazi wa Mbagala Kuu, Edwin Mark (22) Mkazi wa Yombo Vituka na Salim Salehe (45) Mchoraji.

Mashtaka wanayokabiliwa nayo ni kutumia mashine za EFD kwa namna ambayo inapotosha mfumo na kamishna (64) kuisababisha TRA hasara (moja) na kupata usajili wa Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi (TIN) na usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa njia ya uongo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Daisy Makakala, akisaidiana na Auni Chilamula, waliwasomea washtakiwa hao mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Radhamani Rugemalira, na hawakuruhusiwa kujibu chochote.

Washtakiwa hao katika kosa la kwanza hadi la 64 wanadaiwa kutenda kati ya Novemba Mosi na Novemba 30, 2024. Wanatuhumiwa kufanya udanganyifu katika mashine ya EFD kwa lengo la kuupotosha mfumo na kamishna, mashine hiyo mali ya Hadija Songea ikionesha kufanya mauzo na kutoa risiti mbalimbali .

Ilidaiwa kuwa katika shtaka la 65 na 66 linawakabili Mushi, Nanga na Salehe ambao wanadaiwa kupata TIN yenye jina la Hadija Songea kwa njia ya uongo. Wanadaiwa kufanya kosa hilo kati ya Juni Mosi na Juni 30, 2024.

Shtaka la 67, linawakabili mshtakiwa Mushi na Nanga ambao wanadaiwa kufanya udanganyifu kwa kusajili mashine ya EFD kwa jina la Hadija Songea kati ya Juni Mosi na Juni 30, 2024.

Ilidaiwa kwamba katika shtaka la 68, kati ya Novemba Mosi na Novemba 30, 2024 ndani ya mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa waliisababishia TRA hasara ya Sh. 2,160,310,567.51 kutokana na makosa ambayo wameyatenda ya matumizi ya uongo ya mashine ya EFD.

Baada ya kusomewa mashtaka yao, Hakimu Rugemalira aliwaeleza kwamba mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, hivyo hawatakiwi kujibu chochote kuhusu mashtaka hayo. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 20, 2025.

# Aliyetangaza kuuza mtoto Mwanza ashikiliwa na polisi

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linamshikilia John Isaya (21), dereva bajaji na mkazi wa Mtaa wa Bukala, wilayani Sengerema kwa tuhuma za kutengeneza na kusambaza picha mjongeo katika mtandao wa kijamii wa Tik Tok, akitangaza kuwa anauza mtoto wake aliyekuwa amembeba kwa mbeleko kwa Sh. milion 1.6.

Taarifa ya kukamatwa kwa Isaya ilitolewa juzi na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, DCP Wilbrod Mutafungwa wakati anazungumza na vyombo vya habari na kutaja kitendo hicho kuwa ni kinyume cha sheria na ni ukatili kwa mtoto huyo.

Kamanda Mutafugwa alisema kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo kumetokana na taarifa iliyotolewa na Msemaji wa Jeshi hilo Makao Makuu Dodoma, DCP David Misime.

Alisema kuwa taarifa ya DCP Misime ilielekeza mtu huyo atafutwe na akamatwe ili awajibike kisheria kwa kitendo alichokifanya Januari 4, 2025 kilichotweza utu na kukiuka haki ya mtoto huyo.

DCP Mutafungwa alisema kufuatia mahojiano yaliyofanyika dhidi ya mtuhumiwa huyo, chanzo cha tukio hilo ni kutafuta umaarufu kupitia mitandao ya kijamii.

"Tunawakumbusha wananchi kuendelea kufichua vitendo vya kihalifu na waendelee kuvilaani na kuvikemea vitendo vya ukatili wa aina zote kwani vinaweza kusababisha madhara kwa watoto na vinadhalilisha na kushushia thamani utu wao," alisema Kamanda Mutafungwa.

Akikemea tukio la maudhui ya kuuza mtoto juzi, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, aliwataka waandaaji maudhui mtandaoni kuzingatia weledi ili kuepuka uvunjifu wa maadili ya kijamii.

"Jamii ya watanzania inastahili kujipambanua kwa heshima na kuheshimu makundi ya rika zote yanayofanya shughuli mbalimbali za haki mitandaoni, yanastahili heshima na staha," alisema Dk. Gwajima.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mutafungwa alisema jeshi hilo linamshikilia Doto Sita (32), fundi ujenzi na mkazi wa Kishiri, jijini Mwanza kwa tuhuma za kumnajisi na kumlawiti mtoto wake wa kambo mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu hadi kumsababishia umauti.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kutenda ukatili dhidi ya mtoto huyo mara kwa mara huku mama mzazi wa mtoto huyo, akiwa anajua kilichokuwa kinaendelea lakini hakutoa taarifa mpaka wasamalia wema walipotoa taarifa hiyo kwa polisi.

"Raia wema walitoa taarifa hiyo polisi kupitia dawati la jinsia na watoto ambao walifika haraka eneo la tukio na kumkuta mtuhumiwa akishirikiana na mke wake Aneth Mhano (23) kufanya jitihada za kumpeleka hospitalini mtoto huyo ili apatiwe tiba ambako hata hivyo alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema kuwa walifika Kituo cha Afya Usumau ambako walielekezwa kumpeleka mtoto huyo katika zahanati ya serikali Igoma, wakiwa katika harakati za matibabu katika zahanati ya Igoma, mtoto huyo alifariki dunia.

Alisema kuwa mbali na kumkamata mtuhumiwa huyo, pia wanamshikilia na kuendelea kumhoji mama mzazi wa mtoto huyo kwa kutotoa taarifa kwa Jeshi la Polisi au kwa jirani zake juu ya ukatili aliokuwa anafanyiwa mtoto ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Alisema tayari mwili wa mtoto umefanyiwa uchunguzi wa kitabibu na kisha kukabidhiwa kwa baba yake mzazi, Emmanuel Daudi (28) na ndugu wengine kwa ajili ya mazishi na kuwa uchuguzi wa tukio hilo unaendelea na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayebainika kuhusika katika kutekeleza ukatili huo ambao umesababisha kifo.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza wakati akifungua Mkutano wa Tathmini ya Utendaji Kazi wa Nusu Mwaka 2024/25 wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC) jijini Arusha juzi. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Anayedaiwa kuchoma nyumba na kuua watu wanne Tanga, akamatwa Mwanza

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Tanga linamshikilia Mwita Chacha kwa tuhuma za kuchoma nyumba Desemba 30, mwaka jana na kusababisha vifo vya mama na wanawe watatu katika kijiji cha Manga, wilayani Handeni.

Mwita anadaiwa kutekeleza mauaji hayo ya kikatili kutokana na madai kuwa familia ya marehemu Pili Saguge, mama wa watoto watatu, ilimpa sumu mwanawe na kumsababishia kifo.

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, ACP Almachius Mchunguzi jana ilieleza kuwa jeshi hilo lilifanikiwa kumkamata mtuhumiwa mkoani Mwanza alikokimbilia baada ya kufanya tukio hilo.

"Mwita alikamatwa akiwa amejificha jijini Mwanza, na hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa dhidi yake," alisema Mchunguzi.

**SHANGA ZA WIZI**

Alisema kuwa jeshi hilo pia mnamo Januari 6 mwaka huu, saa nane mchana lilimkamata Hamisi Rashidi (21), mkazi wa Majani Mapana, mkoani humo akiwa na vitu ambavyo vinavyodaiwa kuibwa baada ya nyumba ya wananchi kuvunjwa Desemba 16 mwaka jana katika eneo la Uzunguni Kange.

Alitaja vitu hivyo kuwa ni bastola moja aina ya Kevin-ZVI yenye namba H06403, magazine mbili za bastola bila risasi, Laptop mbili aina ya MacBook Air na MacBook Pro, saa sita za mkononi, sime moja, nyundo moja, nondo moja, miwani, funguo mbili, boksi tupu la simu, shanga moja ya kiunoni na sabuni tatu za kuogea ambavyo ni miongoni vya vitu vilivyoibwa siku ya tukio.

"Uchunguzi unaendelea ili hatua zingine za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yake. Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga linaendelea kusisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya wananchi na vyombo vya usalama kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kupitia njia rasmi za mawasiliano.

Alisema jeshi hilo linawahimiza wananchi kuacha tabia ya kuficha wahalifu au kuwapa hifadhi kwa kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika kusaidia wahalifu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Malumbano, matusi ndani ya CHADEMA yana athari mbaya

**CHAMA** cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kiko katika maandalizi ya mwisho ya uchaguzi mkuu ngazi ya taifa. Uchaguzi huo unatarajia kuwapata viongozi wakuu na wale wa mabaraza ya vijana (CHAVITA), Wanawake (BAWACHA) na Wazee (BAZECHA).

Hivi sasa wanaowania nafasi hizo wako katika kampeni za mwisho kushawishi wajumbe kuwachagua ili wawaongoze wanachama na wafuasi wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Pamoja na mambo hayo kuendelea, mvutano mkubwa unaonekana katika nafasi ya mwenyekiti baada ya mwanasiasa machachari, mwanaharakati na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lisuu, kutangaza rasmi na kuchukua fomu kuwania nafasi ya mwenyekiti inayoshikiliwa kwa sasa na Freeman Mbowe.

Kujitokeza rasmi kwa Lissu kuwania nafasi hiyo kumeongeza joto na vuguvugu la uchaguzi huo kuwa kubwa hata kusababisha mgawanyiko miongoni mwa wajumbe na viongozi waandamizi wa chama. Wako waliotangaza waziwazi kuwa wanamwunga mkono Lissu huku wengine wakisema wanasimama na Mbowe katika kinyang'anyiro hicho.

Tangu vigogo hao kuchukua fomu na kuzirejesha, kumekuwa na mgawanyiko mkubwa miongoni mwa viongozi, wanachama na wafuasi na kuwapo kwa kambi mbili za waziwazi. Pamoja na kuwapo kwa mpasuko huo miongoni mwa wanachama, viongozi na wafuasi, pia kumekuwa na kauli na maneno yenye viashiria vya kumega chama katika makundi mawili.

Kila upande umekuwa ukijaribu kutupa maneno ya kejeli dhidi ya upande mwingine. Kambi ya Mbowe, baadhi ya wafuasi wamekuwa wakitoa maneno kama Lissu mropokaji, ana uroho wa madaraka na ametumwa kukivuruga chama kwa maana ya kwamba ni kibaraka wa serikali na chama tawala.


Upande wa Lissu nao umekuja na kauli kadhaa kwamba Mbowe anataka kuwa sultani, hana jipya (kwa maana hana mawazo mapya katika uongozi na maendeleo ya chama), mabadiliko ni lazima na pia lazima kuwe na ukomo wa uongozi. Wafuasi wa kambi hiyo wanaamini kwamba Lissu ndiye atakayeleta mabadiliko ndani ya chama hicho, hivyo ni wakati wa Mbowe kukaa pembeni.

Kwa ujumla, meneno hayo na kejeli ambavyo havina ishara njema ndani ya chama hicho kilichojijengea umaarufu katika medani ya siasa hasa katika mfumo wa vyama vingi. Ni dhahiri kwamba kwa wachambuzi na wafuatiliaji wa masuala ya siasa, huenda kauli, mivutano na kejeli hizo, yakakisambaratisha chama kama hali itaendelea kuwa hivyo.

Mwanasiasa na Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, aliwahi kusema katika siasa hakuna adui wa kudumu waka rafiki wa kudumu. Kwa mantiki hiyo, ni vyema wanasiasa na wafuasi wa kambi hizo mbili zinazovutana wakatambua kuwa kuna maisha baada ya siasa, hivyo waache kutukanana, kukashifiana na kukejeliana.

Mivutano na kutofautiana kwa hoja ndani ya vyama vya siasa na serikali hata katika jamii havina budi kuwapo lakini si kwa kutengeneza maneno ya uhasama na uadui. Uchaguzi ndani ya CHADEMA utapita lazima maisha yataendelea kuwapo, hivyo si vyema kutengeneza uadui katika muda mfupi kama wahenga wasemavyo usiache mbachao kwa msala upitao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# TLP imalize figisu kuna uchaguzi

**NI** zaidi ya miaka 2.5 tangu aliyekuwa mwenyekiti wa taifa wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Augustine Mrema, afariki dunia.

Lakini ni kama chama hicho kimeshindwa kupata mrithi wa nafasi hiyo, kutokana na mgogoro wa kiuongozi unaofukuta.

Ndipo tunapojiuliza itakuwaje wakati uchaguzi mkuu unakaribia? Chama hiki kitashiriki au mambo ni yale yale?

Mrema alifariki dunia mwishoni mwa Agosti mwaka 2022, lakini hadi sasa viongozi wamegawanyika makundi mawili wakiwamo wale anbao wanataka uchaguzi ufanyike na wengine wakipinga.

Picha yenyewe iko hivi; baada ya kifo cha Mrema, Sekreterieti ya TLP ilimchagua mwenyekiti TLP Zanzibar Hamad Mukadam, kuwa Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa.

Mukadam alichaguliwa ili ashikilie nafasi hiyo kwa muda wakati chama kikiendelea na mchakato wa kufanya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama taifa. Lakini hadi leo ni danadana na huku viongozi wakitishiana.

Makundi yanayopingana ndani ya chama hicho ni lile linaloongozwa na makamu Mwenyekiti wa Taifa, Dominatha Rwechungura na la Katibu Mkuu Richard Lyimo, linalopinga kufanyika kwa uchaguzi.

Figisu zilianzia hapa, mara ya kwanza, chama kilipanga kufanya uchaguzi Januari 8 mwaka 2023, ukaahirishwa hadi Machi 6, 2023, lakini ukapigwa danadana hadi Mei mosi mwaka huo ukakwama tena.

Baadaye ukapangwa kufanyika Desemba 28, mwaka huo, lakini haukufanyika, kisha ukapangwa kufanyika Januari 28 mwaka jana, hata hivyo, ukaendelea kupigwa kalenda hadi mwishoni mwa mwezi Juni.

**Ndipo tunapojiuliza itakuwaje wakati uchaguzi mkuu unakaribia? Chama hiki kitashiriki au mambo ni yale yale?**

Hatimaye Juni 29, mwaka TLP chini ya Makamu Mwenyekiti Dominatha ikafanya uchaguzi uliomweka madarakani Ivan Maganza na timu yake, lakini ofisi ya Msajili wa Vyama ikaibuka na kusema haiutambui.

Kwa mujibu wa Dominatha, katika uchaguzi huo Maganza alichaguliwa kwa kura 35, huku wagombea wengine wa nafasi hiyo ya mwenyekiti wa taifa Kinanzaro Mwanga na Stanley Ndamugoba wakiwa na kura 10 kila mmoja, Richard Lyimo na Abuu Changaa wakiambulia sifuri.

Hata hivyo, tangu wakati huo hadi sasa, viongozi hao hawajaingia ofisini kutokana na kile kinachoelezwa kuwa katibu mkuu ambaye nafasi yake ilichukuliwa na mwingine wakati wa uchaguzi anawazuia.

Kwa figisu hizo za zaidi ya miaka miwili, nadhani ipo haja kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iingilie kati kumaliza mgogoro wa kiuongozi ndani ya chama hicho ili kiweze kushiriki uchaguzi mkuu.

Moja ya majukumu ya ofisi hiyo ni kulea vyama vya siasa, hivyo ingekuwa vyema akaziita pande mbili zinazopingana na kuziweka sawa ili chama kiweze kuendelea kufanya shughuli za kisiasa.

Ninaamini katika mazingira ya sasa, si rahisi chama kushiriki uchaguzi au kuzunguka nchi nzima kujiimarisha wakati viongozi hawashirikiani na wanazuiana kuingia ofisi kwa sababu ya mgogoro wa kiuongozi.

Julai mwaka jana, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilikaririwa na vyombo vya habari akitaka vyama hivyo kuepuka migogoro inayojitokeza kwa kuwa inaweza kuleta mifarakano katika taifa.

Akakumbusha kuwa vyama vya siasa ni taasisi, hivyo vinapaswa kusajiliwa na kutenda majukumu yanayotambulika kidemokrasia na kuachana na vurugu zinazosababisha vyama hivyo kuwa na mpasuko.

Kwa kuwa ofisi yake inatambua athari za migogoro katika vyama, ni vyema ikaingilia huo wa TLP ambao sasa una zaidi ya miaka miwili bila kupatiwa ufumbuzi na kusababisha chama kukosa mwenyekiti wa taifa.

Uhai wa chama ni wanachama. Sidhani kwa mgogoro wa kiuongozi unaoendelea TLP chama hicho kinaweza kuwa na wanachama hai na majasiri wanaoweza kusimama na kushindana kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu.

Ipo haja ya ofisi hiyo ya msajili, wana TLP na wadau wapenda demokrasia kukinusuru ili jahazi lisiendelee kuzama na kuleta upweke kwenye harakati za siasa za vyama vingi.

## Bwana harusi anayedaiwa kujiteka apanda tena kortini

**Na Grace Gurisha**

BWANA harusi, Vicent Massawe (36) aliyedaiwa kujiteka mwenyewe amepanda kizimbani kwa mara ya pili katika kesi ya wizi wa gari alilopewa kwa ajili ya kutumia kwenye harusi yake na upande wa mashtaka umedai upelelezi bado haujakamilika.

Massawe alifika jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam akitokea nyumbani baada ya kutimiza masharti ya dhamana ya kuwa na wadhamini wawili na kuwasilisha mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni tisa.

Wakili wa Serikali Aron Titus, alidai kuwa kesi hiyo imeitwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa shauri hilo.

Hakimu Nyaki aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 12, 2025 kwa kutajwa.

Ilidaiwa kuwa Massawe ni mfanyabiashara na mkazi wa Kigamboni, katika shtaka la kwanza anatuhumiwa kuiba kama wakala. Inadaiwa Novemba 15, 2024 akiwa eneo la Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam, aliiba gari hilo alilopewa na Silvester Beda kwa jili ya kulitumia kwenye harusi yake.

Inadaiwa gari hilo aliloazimwa alitakiwa kulirudiaha, lakini hakufanya hivyo, thamani yake ni Sh. milioni 15 mali ya Beda.

Katika shtaka la pili, Massawe siku hiyo hiyo na eneo hilo anatuhumiwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu Shilingi milioni tatu kutoka kwa Beda akiahidi kwamba atarudisha huku akijua si kweli.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo alikana kuhusika na tuhuma hizo.

Awali, Massawe alidai kuwa gari ambalo anatuhumiwa kuliiba namba T 642 EGU Toyota Ractis ni la kwake na kwamba nyaraka zote anazo na kuiomba mahakama gari hilo liletwe mahakamani kama dhamana yake.

"Gari hili lililotajwa kwamba nimeliiba si kweli, gari ni langu, lakini taarifa iliyotolewa na kusambaa inadai gari sio langu, naomba gari liletwe kama dhamana yangu hapa mahakamani," alidai Massawe.

Aliendelea kudai kwamba katika suala la dhamna hilo atalitimiza kwa sababu mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni tisa ipo.

"Polisi walichelewa kunipa taarifa kuwa wananileta mahakamani, nikachelewa kutoa taarifa, lakini nimeshamwambia mke wangu yupo njiani anakuja hapa," alidai Massawe. "Bahati mbaya nilishatoa masharti ya dhamana kwamba mali isiyohamishika hiyo unaweza ukaitumia kama kielelezo," alisema Hakimu Nyaki.

Hakimu Nyaki alimweleza mshtakiwa ili awe nje kwa dhamana anatakiwa awe na wadhamini wawili wenye vitambulisho vya NIDA watakaosaini bondi ya Shilingi milioni tano na pia atatakiwa kuwasilisha mahakamani fedha taslimu au mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni tisa.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mema Asep Learning Centre iliyopo Kisarawe mkoani Pwani wakiwa katika mafunzo ya kutengeneza mafuta ya mgando yaliyotolewa na kampuni ya Matungullu's Product hivi karibuni, kwa lengo la kuwapa ujuzi wa kujiajiri wanapohitimu masomo yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maabara ya kisasa madini kujengwa mkoani Dodoma

**Na Valentine Oforo,**
DODOMA

WAKALA wa Jiolojia Tanzania (GST) unatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa maabara ya kitaifa ya kisasa ya madini jijini Dodoma.

Mradi unaotarajiwa kuanza kutekelezwa mapema mwezi ujao katika eneo la Kizota, ni sehemu ya jitihada za GST za kuongeza ufanisi na tija ya sekta ya upimaji wa madini nchini.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Mkurugenzi wa Huduma za Maabara wa GST, Notka Banteze, alisema maabara hiyo ya kisasa ya ghorofa moja itatumika kama kituo cha rufani cha kupokea sampuli za madini kutoka kanda zote nchini na nchi za jirani.

Alisema ujenzi wa maabara hiyo ya kisasa utajumuisha sehemu kuu mbili, ikiwemo ofisi za wataalamu, sehemu ya kemikali na petrolojia na madini pamoja na sehemu ya usindikaji wa madini.

"Maabara itakuwa na maabara zingine ndogo zitakazojikita na uchunguzi wa mambo mbalimbali zikiwamo maabara ya usindikaji wa madini, maabara ya jioteknolojia, maabara ya jiokemia, petrolojia na maabara ya mazingira ili kutoa huduma pana kwa wadau wa madini nchini," alisema.

Mbali na kuhudumia wadau wa madini wa ndani ya nchi, Banteze alibainisha kuwa maabara itajengwa kwa hadhi ya juu ili kuhudumia wadau wa madini kutoka nchi jirani.

"Tanzania kupitia GST imeidhinishwa na Shirika la Ithibati la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAS) kama chanzo cha uhakika cha upimaji wa sampuli za madini, hali ambayo imekuwa ikiwavutia wadau kutoka nchi mbalimbali kuleta sampuli zao za madini kwa ajili ya uchunguzi," alisema.

Alisema hadi kufikia Desemba, mwaka jana, GST ilipokea sampuli za madini kutoka nchi kadhaa zikiwemo Kenya, Uganda na Sudani.

"Uganda, kwa upande wao, wameleta maombi maalumu ya kushirikiana na GST katika swala zima la upimaji wa madini, hatua ambayo inathibitisha namna ambavyo Tanzania, kupitia GST tumepiga hatua kubwa katika sekta ya upimaji madini," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imeendelea kuwekeza jitihada na fedha za kutosha kuendeleza ufanisi wa shughuli za wakala, hali ambayo inashuhudia ufanisi mkubwa.

"Kwa sasa, tuko katika mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha tunasogeza huduma zetu kwenye kanda zote zenye shughuli za madini hapa nchini," alisema.

Alisema ujenzi wa maabara ya Dodoma utakwenda sambamba na ujenzi wa maabara nyingine katika miji ya Geita na Mbeya na maabara zingine zinatarajiwa kujengwa Lindi, Tanga na Mpanda.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# TCRA yaandaa Mpango Kitaifa wa Mawasiliano kwenye maafa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeandaa na kuchapisha Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura unaoainisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuwasiliana katika kipindi cha maafa.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, aliyasema hayo hivi karibuni, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi kuhusu mpango huo.

Alisema mpango mkakati huo unakusudia kutambua uwezo unaohitajika kwa watoa huduma za dharura na namna ya kuwasiliana katika hatua zote za usimamizi wa maafa.

Alisema kuwa lengo ni kuhakikisha kuwapo utangamani wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano wakati wa dharura.

Aidha, alisema unakusudiwa kutambua uwezo wa watoa huduma za dharura kimawasiliano na pia vikwazo katika usambazaji mifumo ya mawasiliano.

Maafa ni tukio lisilotarajiwa linalosababisha uharibifu, maangamizi na mateso makubwa ya kibinadamu ambayo yako nje ya uwezo wake. Kwa hali hii waathirika wanahitaji msaada wa nje ngazi ya kitaifa au kimataifa.

Mpango huo unatarajiwa kufanikisha mawasiliano wakati wa maafa kama mafuriko ya Rufiji na Hanang na kuporomoka kwa jengo la biashara Dar es Salaam ambako watu kadhaa walipoteza maisha.

Kwa mujibu wa Dk. Bakari, mpango huo unaelezea namna ya kudhibiti vihatarishi kwa kuimarisha mawasiliano kwenye hatua zote za shughuli za kiserikali, za umma, sekta binafsi na za jamii iliyoko kwenye vihatarishi husika.

Vilevile, unasisitiza umuhimu wa kuchambua vihatarishi muhimu vya miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

"Miundombinu hii inaweza kuathiriwa na maafa ya asili, mafuriko, kukumbwa na vimbunga au shughuli za kibinadamu na hujuma," alisema.

"Vihatarishi ni jambo au kitu chochote kinachoweza kwenda mrama na kuleta athari hasi zinazoweza kusababisha maafa. Mpango wowote wa kudhibiti vihatarishi unatakiwa kuweka utaratibu wa kuvipunguza, kufanya maandalizi ya kukabiliana navyo vinapotokea na kurejesha hali ya awali," alisema.

"TCRA itazingatia mahitaji na kuharakisha utoaji wa leseni zitakazofanikisha usimamizi wa maafa na masuala ya dharura. Leseni hizo ni pamoja na masafa, namba na idhini ya vifaa vya mawasiliano vinavyoruhusiwa kutumika Tanzania," alifafanua Dk. Bakari.

Aidha, lengo ni kuhakikisha kwamba huduma zinazowezeshwa na miundombinu ya mawasiliano iliyoathiriwa na maafa zinarejeshwa ndani ya saa 24 na mpango huo unawataka wadau kufanya mafunzo ya mara kwa mara ya namna ya kushughulikia vikwazo vya mawasiliano wakati wa majanga na maafa.

Vilevile, wanatakiwa kuwa na utaratibu wa kutambua, kuchambua na kuchukua hatua kuimarisha njia za mawasiliano ili ziendelee kutumika wakati wa maafa.

Alisema TCRA inapitia mpango huo kila baada ya miaka mitatu na kuuboresha. Hatua hii itazingatia maendeleo ya teknolojia za mawasiliano na uzoefu kwenye kusimamia maafa.

# Zaidi ya vijana 100 waanzishiwa biashara

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

VIJANA 104 waliokuwa kwenye hatari ya kujiingiza katika makundi hatarishi ya vitendo visivyo faa kwenye jamii kutokana na kukosa shughuli za kufanya, wameanzishiwa biashara ya kuwaingizia kipato ili kuendesha maisha yao.

Baadhi ya biashara hizo ni pamoja na bucha za samaki, mabwawa ya kufugia samaki, kukaanga samaki na kuku pamoja na kumiliki migahawa ya kuuza vyakula na vinywai vya aina mbalimbali.

Wanafuika hao wakiwamo wa kike na kiume wanatoka katika kata ya Mzumbe na Mlali, Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, wamewezeshwa na Shirika la Youth Power Organization (YPO) kwa kushirikiana na mradi wa Skills for Employment Tanzania (SET) unaotekelezwa na Shirika la Swisscontact Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa YPO, Charles Makongo, alisema hayo wakati akihitimisha mradi huo uliofadhiliwa Ubalozi wa Uswisi Tanzania kupitia Mradi wa Ufugaji Samaki na Ujasiriamali, unaendeshwa na shirika hilo.

Alisema mradi hou ulianza Machi, mwaka jana na kuwafikia vijana 170 kwa kuwapa mafunzo ya siku 32 yaliyokuwa pia yana mchujo aina mbalimbali ili kuwapata vijana sahihi kwaajili kuendesha biashara zao na kujiingizia kipato.

Mkurugenzi Makongo, alisema kundi hilo la vijana 104 wakiwamo wasichana na wavulana walionyesha jitihada mbalimbali na nidhamu za kutaka kufanikiwa kama vijana na kupatiwa vitendea kazi.

"Tumefanikiwa kuwa na vijana wanaomiliki mabwawa yao ya samaki na wanafuga kibiashara, wapo vijana waliofungua mabucha yao ya samaki na tayari wameanza kuingiza pesa, wapo wanaofanya biashara ya kukaanga samaki na kuku pamoja na wengine wanamiliki migahawa ya kuuza chakula kwa kutumia mboga ya samaki na kuku," alisema.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirika la la Swiss contact Tanzania, Masunga Isumbi, alisema mradi wa SET umelenga kuwafikia vijana wa kiume na kike ambao walipata ujauzito kwenye umri mdogo kuzia miaka 15 hadi 24 kwa Mkoa wa Morogoro na wilaya zake zote.

Alisema mradi huo umeshirikiana na Taasisi ya Youth Power Organization ambao ulilenga kuwafikia vijana 170 wa ufadhili wa Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania na kufanya kazi na Taasisi 13 za mkoa huo.

Vijana walionufaika na mradi, Mohamed Said Abdallah alisema kupitia mradi huo umemwezesha kuwa na bwawa la kufugia samaki na kuheshimika mtaani kwa kuwa mwanzo walikuwa wakionekana kama vijana wasio na shughuli huku baadhi ya watu wakiwahusisha na vitendo visivyofaa katika jamii.

Neema James, mnufaika mwingine wa mradi huo, alisema umewawezesha kufungua mgahawa wa kuuza vyakula huku kitoweo kikiwa samaki na kuku na kujiingizia kipato kwa siku, ambacho kinaendesha maisha yao tofauti na awali walikuwa mtaani bila shughuli za kufanya.

Akihitimisha mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Mwalimu Linno Mwageni, alisema vijana hao watapata fursa mbalimbali ikiwamo kuanzishiwa vitalu vya vifaranga vya samaki pamoja kupewa miche ya miti ya michikichi, karafuu na kakao, bure.


**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA**

**CONTAINER SPACE SOLUTIONS TANZANIA LIMITED**

**Cheti cha Usajili No. 118987**

Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni CONTAINER SPACE SOLUTIONS TANZANIA LIMITED, yenye usajili namba 118987 kitakachofanyika tarehe 25 Januari 2025 ofisini kwa mfilisi saa 4:30 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi | LINDA ALLAN MWAMBETE |
| Amwani ya Mfilisi | 368 MSASANI ROAD<br>MIKUMI HOUSE<br>OYSTERBAY<br>P.O BOX 9673<br>DAR ES SALAAM<br>TANZANIA |
| Tarehe ya kuchaguliwa | 13 NOVEMBA 2024 |
| Amechaguliwa na | WAMILIKI WA KAMPUNI |

Sahihi ............................................ Tarehe: 24/12/2024

Jina: LINDA ALLAN MWAMBETE

118315302


## Huduma soko la Tandale kuwa saa 24

**Na Pilly Kigome**

KATIBU Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Toba Nguvila, ametoa siku 14 kero zote zinazowakabili wafanyabiashara wa soko la Tandale zifanyiwe kazi na kukamilika ili lianze kutoa huduma kwa saa 24.

Pia amemwagiza Katibu Tawala wa Wilaya ya Kinondoni na Mkuu wa Wilaya hiyo, wakae mezani na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) kuanza kwa ruti mpya ya mabasi ya abiria yatakayoingia sokoni hapo ili soko lifikiwe kwa urahisi hatimaye kuchochea ongezeko la mapato kwa soko hilo.

"Leo (juzi) Jumatatu Januari 6, 2025 nataka hadi ikifika Ijumaa ya Januari 10, mnipe majibu mniambie ruti hii itaanza lini sokoni hapa," alisema Dk. Nguvila wakati wa mwanzo mwa ziara yake ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika halmashauri zote tano za mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika soko hilo kwa ajili ya kuwezesha maendeleo kwa wananchi ni lazima kuendane na hadhi ya uwekezaji huo.

Pia alitaka kuwapo kwa uhitaji mkubwa wa huduma kwa watumiaji wa soko hilo kwa kuwa bidhaa zingine zinaingia usiku huku baadhi ya wanunuzi wakitoka mbali, hivyo kulazimika kusubiri huduma asubuhi jambo linalofanya kuwa kero kwa wateja na wadau.

Katibu Tawala pia aliagiza kutolewa kwa taa zilizowekwa sokoni hapo ambazo zimelalamikiwa kuwa hazina mwanga wa kutosha na kuwekwe taa zingine kubwa zitakazokidhi mahitaji, kununuliwe jenereta kubwa litakalohudumu na kukidhi wafanyabiashara wote sokoni hapo saa 24 hata kama umeme utakatika.


Agizo lingine alilotoa ni kununuliwe pampu ya kuvuta maji kuondoa kero iliyopo kwa kukosekana kwa maji sokoni hapo na kuondoa maji yanayoingia katika baadhi ya vizimba mvua inaponyesha.

Mweka Hazina Manispaa Kinondoni, Onesmo Mwonga, alisema soko hilo likikamilika kama ipasavyo, litaingiza mapato ya Sh. milion 2.5 kwa siku.

Baadhi ya wafanyabiashara hao walilalamikia mwanga hafifu, ukosefu wa barabara kuingia kwa magari na kuingiliwa na maji inyeshapo mvua hali inayofanya kuwa kero kwa jengo hilo jipya pamoja na ukosefu wa vyoo ghorofa ya chini.

Katika ziara hiyo, Dk. Nguvila alikagua Kituo cha Afya Kinondoni ambacho kimekamilika na kuanza kutoa huduma za mama na mtoto, maabara, wagonjwa wa nje na meno. Hadi sasa kituo hicho kina watumishi 32 na kuwa na upungufu wa watumishi 20 ambao tayari kibali cha kutoa ajira kimeshatoka.

Pia alikagua mradi wa jengo jipya la Manispaa ya Kinondoni ambalo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 98, hivyo kuagiza mkurugenzi na meya wahamie mara katika jengo hilo. Aliagiza pia idara zingine ambazo hazijahamia rasmi katika jengo, kufanya hivyo na waangalie jengo la zamani watalitumiaje ili kuingiza mapato.





## ‘Wanaotorosha korosho nje ya nchi wahujumu uchumi’

**Na Oscar Assenga,** TANGA

BODI ya Korosho Tanzania (CBT) Mkoa wa Tanga inatarajia kuwachukulia hatua wakulima watakaokamatwa kwa tuhuma ya kuchepusha zao hilo na kuuza nje ya nchi kinyemela kwa kosa la uhujumu uchumi.

Meneja wa CBT, Mkoa wa Tanga, Atufigwege Mwakyagi, alitoa kauli hiyo jana katika mahojiano yake maalum na Nipashe.

“Tutashughulika nao wanaohujumu zao hili kwa sababu korosho ni zao la kimkakati la kitaifa, serikali inawekeza juhudi kubwa ili kuongeza uzalishaji lengo kuwanufaisha wakulima na taifa,” alisema Mwakyagi na kuongeza:.

“Hao dawa yao iko jikoni. Hatutawafumbia macho tutakapo wabaini watakamatwa na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria ili kudhibiti hali hiyo inayochangia kurudisha nyuma jitihada za serikali.”

Alisema juhudi zinafanyika kudhibiti utoroshwaji wa korosho mkoani hapa katika mpaka wa Tanzania na Kenya.

Kuhusu mnada, Mwakyagi, alisema unatarajiwa kuanza mwezi huu baada ya wakulima kupeleka korosho zao kwenye vyama vya msingi kisha ghalani.

Alisema mkoa huo na bodi, wanashirikiana na vyama vikuu vya zao la korosho, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mrajisi wa Mkoa ili kujua taratibu za kutangaza mnada huo.

Alisema kinachokifanya kwa sasa ni kuhamasisha wakulima kuendelea kupeleka korosho kwenye vyama hivyo na baadaye ghala kuu.

Kuhusu wakulima kupeleka korosho isiyokuwa na ubora alisema,“Korosho zipo kwenye madaraja mawili; la kwanza na la pili.

“Tunasisitiza wakulima wazingatie ubora kwa sababu tofauti na ubora korosho haziwezi kupata bei nzuri,” alisema Mwakyagi”

**“Hao dawa yao iko jikoni. Hatutawafumbia macho tutakapo wabaini watakamatwa na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria ili kudhibiti hali hiyo inayochangia kurudisha nyuma jitihada za serikali.”**

# Mtoto wa Kitanzania aandika historia Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MVULANA wa Kitanzania, Anwaar Njiku (10), Mkazi wa Njiro jijini Arusha ameandika historia ya kuwa mtoto mdogo zaidi wa kwanza kuwahi kufika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro.

Anwaar, alipanda mlima huo mrefu zaidi barani Afrika kwa siku nane, akitumia lango la Lemosho (Siha) na kuteremkia lango la Mweka.

Akizungumza jana baada ya kutimiza ndoto hiyo, mvulana huyo alisema safari yake hiyo ilianza Desemba 29, mwaka jana na kuhitimisha Januari 5, mwaka huu, majira ya saa 12 asubuhi.

Kwa kawaida, safari ya kupanda Kilimanjaro humpitisha mpandaji katika kanda za hali ya hewa tofauti, kuanzia ile ya nchi za tropiki hadi arktiki.

Kilele cha Kibo chenye urefu wa mita 5,895, ndicho kivutio kikubwa kwa wageni kutokana na kufunikwa na theluji.

Ni kivutio kikubwa cha watalii kutokana na mandhari yake ya kipekee, mifumo ya eco-diversity, na fursa za kupanda mlima.

Kilimanjaro unajivunia njia mbalimbali za kupanda, na vivutio vyake ni pamoja na barafu (glaciers) za Uhuru Peak, hifadhi ya wanyama, na misitu ya mvua.

Katika orodha ya milima mikubwa duniani, Kilimanjaro unashika nafasi ya nne kwa urefu.

Katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), kuna njia sita za kupanda hadi kileleni na njia iliyo rahisi, na iliyo maarufu zaidi ni ile ya kuanzia lango la Marangu, ambako ndiyo makao makuu ya hifadhi.

Baba mzazi wa mvulana huyo, Athuman Njiku, alisema Anwaar, alipanda Mlima huo, akiongozana na watalii 10 kutoka nje ya nchi, kama sehemu ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Kwa mujibu wa Kanzidata ya KINAPA, Anwaar, ndiye mtoto mdogo zaidi wa Kitanzania kufikia kwenye kilele hicho. Mlima huo una urefu wa mita 5,895 (19,341 feet) kutoka juu ya usawa wa bahari.

Anwaar, ameandika rekodi akijaribu kufuata njia iliyochongwa na msichana wa Kitanzania, Rawan Dakik (20), ambaye naye alivunja rekodi ya kupanda kilele cha Mlima Everest Juni mwaka 2021.

Rawan, alipanda milima mikubwa sita duniani iliyopo katika mabara sita kati ya saba; ambayo ni Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5,895, Elbras ulipo Urusi ( 5,648), Aconcagua wa Argentina (6,961), Carstenz Pyramid wa Indonesia (4,884), Vinson Massif wa Antarctica (4,8920 na Mlima Everest wa Nepal (8,848).




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, akimtwisha ndoo ya maji mama katika kata ya Arri iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara baada ya kuzindua mradi wa maji juzi, wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2 uliofadhiliwa na Shirika la Karimu Foundation ambao utahudumia zaidi ya wananchi 3,000. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Wananchi Arri waaga kero ya maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ZAIDI ya wakazi 3,000 wa Kata ya Arri wilayani hapa Mkoa wa Manyara wameanza kunufaika na mradi wa maji uliojengwa na Shirika la Karim Foundation.

Jana, Mkurugenzi wa Shirika hilo, Shau Erro, alimweleza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo kuwa tangu kusanifiwa na kujengwa kwa mradi huo hakuna mwananchi anayefuata maji umbali wa zaidi ya mita 400.


“Huu mradi tumetumia shilingi bilioni 2.482, wananchi wa Arri wamechangia shilingi milioni 128 kama nguvu kazi, ikiwemo kuchimba mitaro na shughuli nyingine za ujenzi,” alisema Erro.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Manyara, James Kionaumela, alisema mradi huo umeongeza upatikanaji wa majisafi na salama wilayani hapa hadi kufikia asilimia 83.

Akizungumza baada ya kuzindua mradi huo, Waziri Mkumbo, aliwapongeza wahisani hao kwa upendo wao na jitihada za kuchangia maendeleo ya jamii.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wanamtua mama ndoo kichwani, huku akisisitiza miradi kama hiyo, ni hatua kubwa kuelekea kufanikisha lengo hilo.

Akitoa shukrani kwa niaba ya wananchi, Mbunge wa Babati Vijijini na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, aliwashukuru wahisani na serikali kwa kuhakikisha wanapata huduma bora za maji.





# Serikali yaagiza maboresho ufundishaji sayansi, hisabati

**Na Restuta Damian,**
KAGERA

SERIKALI imewaagiza walimu wa hisabati, sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kufanya maboresho katika ufundishaji ili kuinua kiwango cha ufaulu wa masomo hayo kwa wanafunzi nchini.

Agizo hilo limetolewa juzi na Mratibu wa Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SQUIP) wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Richard Makota wakati akizungumza na walimu zaidi ya 1,000 wanaoshiriki mafunzo ya kubadili ufundishaji wa masomo hayo nchini.

Makota, alisema ili kuhakikisha wanafunzi wanapenda masomo hayo na kuyafaulu, lazima walimu wabadili utaratibu wa kufundisha na kuja na mbinu mbadala ili kuwajengea zaidi ufahamu.

"Kwa jinsi tunavyokimbia na maendeleo ya teknolojia nchini, tunahitaji kuacha mfumo wa ufundishaji uliozoeleka na kuja na mbinu mbadala ili kuwa na matokeo chanya," alisema Makota.

Alisema kupitia mafunzo hayo, serikali inatarajia walimu hao kurejea shuleni na kufanya mabadiliko kwa kutengeneza vipindi vya kuwawezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo hayo na mitihani yao.

Makota, alisema wanatarajia kufanyika mambo makubwa matatu ambayo ni kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa sayansi, kupata wataalamu wengi kusaidia kuinua teknolojia nchini na masomo hayo kuwa idadi kubwa ya wanafunzi.

Mwenyekiti wa Wawezeshaji, Winchslaus Bilige, alisema walimu wa sayansi wana jukumu la kuwasaidia wanafunzi wa masomo hayo kwa kutumia mbinu walizopewa kwenye mafunzo hayo.

Bilige, alisema matarajio ya TAMISEMI kwa kutumia mafunzo hayo, ufaulu wa masomo hayo kufikia asilimia 50 kwa 50 kwa wanafunzi wa kike na kiume nchini.

Alisema ili kufikia azma hiyo ni lazima mwalimu akubali kubadilika katika uandaaji wa vipindi vyake.

Ofisa Elimu Mkoa wa Kagera, Marco Kigola, alisema ufaulu wa wanafunzi kwa kidato cha nne, pili, darasa la saba na nne mwaka juzi ulifikia asilimia 100.

Kigola alifafanua kuwa kidato cha nne wanafunzi walifaulu kwa asilimia 82, cha pili 79, darasa la saba 70 na la nne 84.



Mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa barabara wa uboreshaji wa miundombinu ya miji Tanzania (TACTIC) katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, akiendelea na ujenzi wa mitaro ili kuzuia maji kutuama na kuingia katika makazi ya wananchi na kusababisha mafuriko katika mtaa wa Nyasubi jana.**PICHA; SHABAN NJIA**

## Ugawaji vyandarua kuanza Jan. 16 Shy

**Na Marco Maduhu,**SHINYANGA

VYANDARUA vyenye dawa milioni 1.5 vinatarajiwa kusambazwa kwa wakazi mkoani hapa kukabiliana na ugonjwa wa malaria Januari 16, mwaka huu.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Mwandamizi wa Wizara ya Afya, Peter Gitanya wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Gitanya, alisema vyandarua hivyo vinasambazwa kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP), ikiwa ni kampeni ya taifa ya kutokomeza ugonjwa huo nchini ifikapo mwaka 2030.

"Mkoa wa Shinyanga vyandarua milioni 1.5 vitasambazwa na kaya zote zitafikiwa, kwa sasa tupo kwenye uandikishaji kaya kwa kaya, na chandarua kimoja watapewa watu wawili wawili kwa kila Kaya," alisema Gitanya.

Alisema kaya ambayo haitaandikishwa kuanzia Januari 2 hadi 15, mwaka huu haitapewa chandarua ugawaji huo utakapoanza Januari, 16.

Aliwataka wakazi hao kuchukua hatua stahiki mpaka watakapopata kadi maalumu kwa ajili ya kupewa chandarua.

Kuhusu hali ya malaria nchini, alisema Shinyanga inashika nafasi ya nne kitaifa kuwa na kiwango cha juu kwa asilimia 16.

Tabora nafasi ya kwanza kwa asilimia 24, ya pili Mtwara 20, na ya tatu ni Kagera 18. Hali ya ugonjwa huo kitaifa ni asilimia nane.

Happines Nania kutoka Wizara ya Afya, alisema kwa mwananchi ambaye atapoteza kadi ambayo alipewa wakati akiandikishwa kwa ajili ya kupewa chandarua, anapaswa kwenda kituo husika ili apewa chandarua chake kwani taarifa zake zitakuwepo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Faustine Mlyutu, aliwaomba waandishi wa habari kushiriki kikamilifu katika kampeni hiyo ya mapambano dhidi ya malaria.

"Tumieni kalamu zenu kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya vyandarua vyenye dawa ili tuijenge Shinyanga isiyo na malaria,"alisema Mlyutu.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga, Greyson Kakuru, alisema ushirikishwaji waandishi wa habari katika kampeni hiyo utasaidia kupeleka ujumbe sahihi kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya vyandarua hivyo vyenye dawa kukabiliana na malaria.

# DC awataka wenyeviti mitaa kuacha ubaguzi

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Edward Gowele amewataka viongozi wa serikali za mitaa na vijiji wilayani hapa kuacha ubaguzi na upendeleo wakati wa kutatua kero za wananchi.

Gowele alitoa rai hiyo juzi wakati wa mafunzo elekezi ya utawala kwa viongozi hao baada ya kushinda katika uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba mwaka jana.

Alisema viongozi hao wana wajibu wa kusimamia utatuzi wa migogoro kwenye maeneo yao kwa njia za amani, endapo watashindwa wawasilishe katika vyombo vya juu vya sheria ili kupata suluhu

"Nendeni mkasimamie utatuzi wa migogoro maeneo yenu bila upendeleo wala uonevu na kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma na haki zake kwa wakati mahali popote alipo," alisisitiza Gowele.

Alivitaja vipaumbele vya utawaka katika wilaya hiyo kuwa ni pamoja na kuimarisha elimu kwa kuhakikisha watoto wote wanaostahili kuanza darasa la kwanza, wanaandikishwa na kupelekwa shule na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara aliwataka viongozi hao kuepuka matumizi mabaya ya madaraka kwa kudai na kupokea rushwa na kuwahudumia wananchi bure.

"Msitumie mihuri ya ofisi zenu vibaya kwa kuwanyanyasa wananchi wanyonge, toeni huduma kama watumishi wa watu huku mkisimamia miradi ya maendeleo na kuleta maisha bora kwa wakazi wa maeneo yenu," alisema Waitara.

Baadhi ya viongozi hao, akiwemo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ng'ereng'ere, Chacha Amiri alishauri halmashauri kuweka mikakati ya kuwalipa posho ya mwezi kutoka mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi kwa wananchi wakati wa kutekeleza majukumu yao.

"Viongozi wa vijiji na mitaa hawana malipo yanayoeleweka serikalini, wanatekeleza majukumu yao kwa kujitolea, tunashauri halmashauri itumie mapato ya ndani kuwalipa posho kila mwezi," alisema.




Ukurasa 13

**JOTO UCHAGUZI NDANI YA CHADEMA NI MAKUNDI TIMU MBOWE, LISSU**



Ukurasa 14

**MUHTASARI DIRA 2050 (1)**



## BUNDI MVURUGA CHADEMA

# Mchambuzi awasihi Lissu, Mbowe wasimkaribishe

• Ataka wauache munkari, wajadili

**Na Sabato Kasika**

CHADEMA inaendelea na mchakato wa kujiandaa na uchaguzi wa viongozi wa safu ya juu baadaye mwezi huu, lakini vita vya kuwania uongozi kati ya mwenyekiti na makamu wake wanaogombea nafasi moja, vinawaibua washauri wanaowataka kupunguza kutuliza munkari.

Ni Januari 21 atakapochaguliwa Mwenyekiti Taifa na Makamu wake, wakati huu njia zote zikielekea kwenye uchaguzi huo, wanachama na wafuasi wamegawanyika makundi mawili.


Ni walio upande wa Mwenyekiti wa sasa Freeman Mbowe na wale wanaomuunga Makamu Mwenyekiti Tundu Lissu.

Hatua hiyo inatokea baada ya miamba hiyo miwili kuchukua fomu kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa na kusababisha kuwapo kwa mgawanyiko huo.

Kuwapo mazingira hayo, mchambuzi wa siasa anayechipukia, Pawa Lufunga, anakuja na ushauri kwa chama hicho kwa lengo la kutaka kivuke salama kwenye uchaguzi ujao.

Pawa anashauri, ifanyike meza ya mazungumzo, wazee wa chama na washauri wa chama wakae nao kabla ya uchaguzi ili kuweka mambo sawa, kuwa na dira moja itakayosaidia kudhibiti makovu yanayoweza kujitokeza katika uchaguzi unaokuja.

"Lakini pia ni muhimu Lissu kuongozwa na hekima zaidi kwani yeye ni mgombea na si




Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe akiwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama Edward Lowassa, (marehemu) baada ya kuchukua fomu ya kugombea urais 2015. Lowassa ni miongoni mwa vigogo maarufu Mbowe aliowavuta.**PICHA: MTANDAO.**

mshindi, hivyo huenda asishinde, ikitokea hajashinda maisha yake mbele ya viongozi aliowanyooshea vidole ili aweze kuongozwa nao itamlazimu kuwa na hekima zaidi," anasema.

Anasema hekima isipotumika ataamua aidha kudai amehujumiwa na kutumia nguvu ya kitaaluma ya sheria kuwapeleka mahakamani ambako huenda kukawa na anguko kubwa la chama.

Mchambuzi huyo anaongeza kuwa hali hiyo huenda pia ikatumiwa si tu kuangamiza chama bali kumwangamiza yeye mwenyewe, kwa kuwa katika historia anabaki kuwa sehemu ya wakosoaji wakubwa wa serikali wanaohofiwa kusumbua watawala.

"Kwa maana hiyo, ninarudia tena kuwe na meza ya mazungumzo kumaliza changamoto iliyopo, lakini pia hekima inahitajika kwake na kwa wale anaowanyooshea vidole ndani ya chama chao ili kusaidia kukivusha kuanzia wakati huu hadi wa uchaguzi," anasema Pawa.

Mchambuzi huyo anasema hakuna wakati mbaya na wa hatari kwa chama cha siasa kama wa uchaguzi, uwe wa ndani au nje ya chama kupata viongozi au makada wake wa kukipambania na kuvikabili vyama vingine.

"CHADEMA msikumbwe na tatizo hilo, kwani vyama vingi katika historia ya dunia vimepotea katika vipindi vya uchaguzi, yaani wakati wa kuteua wagombea kuchuana na wa vyama vingine katika nafasi ya urais, ubunge na udiwani au katika uchaguzi wa ndani," anasema mchambuzi.

Pawa anafafanua kuwa mgongano wa maslahi baina ya wanaharakati, kukosekana kwa fursa za kufikia malengo na kunyimwa fursa za kukua kisiasa huwaondoa wanasiasa katika vyama vyao.

"Watu wenye ushawishi mkubwa wakiondoka, hubomoa chama kwani huondoa wafuasi wa chama wanaoamini katika siasa zao na hivyo kuzorotesha chama. La muhimu CHADEMA Mungu awanusuru," anasema.

Pawa anaamini kuwa ushauri wake ukifanyiwa kazi, chama hicho kinaweza kuvuka salama katika mnyukano huo unaoendelea ambao umewagawa wanachama makundi mawili.

"Vyama vingine vinaweza kutumia mnyukano huo kupenyeza sumu ya kukisambaratisha kwa kuchochea mgogoro ambao hautafikia mwisho na kujikuta CHADEMA inakosa nguvu zama hizi za kuelekea kwenye uchaguzi mkuu," anasema.

Anasema migogoro ndani ya vyama ni sumu ya maendeleo ya vyama vyenyewe na kwamba chama hicho kisuruhusu kuwapo kwa hali kama hiyo itakayokinyong'onyeza na kukidhoofisha.

**NGUVU MBOWE, LISSU**

Mchambuzi huyo anasema Mbowe na Lissu ndio wanasiasa wenye ushawishi zaidi katika chama hicho kwa sasa, tena ni viongozi wa juu zaidi wenye wafuasi wengi ndani na nje ya CHADEMA.

Anasema ushawishi wao unawafanya wote kuwa watu muhimu, na kwamba wanahitajika ndani ya chama, huku Lissu, akiendesha kampeni ngumu kwa ustahimilivu wa chama.

"Lakini wengi hasa wa mashabiki na wafuasi hawawezi kuliona hili kutokana na umahiri wa Lissu katika kujenga hoja hasa za kukosoa, alianza kwa kukosoa chama chake, akiwa mmoja wa viongozi wa juu zaidi chamani, amekuwa akiibuka hadharani kulalamika juu ya kutokuridhishwa na miendendo ya ndani ya chama," anasema.

Anaongeza kuwa hali inakuwa ngumu zaidi pale Lissu anaposimama hadharani kuhoji na kukosoa usimamizi wa fedha za chama, na kwamba amekwenda mbali na kudai kuwa viongozi wenzake wanahongwa pesa huku akiwataja kwa majina baadhi yao.

"Kukataa hadharani kwa maridhiano ya chama hicho na serikali, kuwashutumu wenzake kwa majina kuwa wamehongwa na watu wa serikali, kuibua tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za chama ni mambo yanayofanya Lissu asiposhinda uenyekiti na wale anaowatuhumu wakashinda itakuwa ngumu kwake kudumu chamani," anasema.

Anaongeza kuwa uamuzi huo inawataka wanachama kuwa na hekima zaidi, kwa kuwa wanaweza kujikuta wanamuona kama mpinzani ndani yao na kuanzisha nguo taasisi na wakaamua kumshughulikia kama muasi wa chama.

Anaonya kuwa hali hiyo inaweza kuzorotesha demokrasia yao na kuonyesha kuwa anashughulikia kwa kushindana na Mbowe.

# Carter kuzikwa kesho, ameifanyia mengi Afrika



Marais Jimmy Carter (kushoto) na William Tolbert wa Liberia wakisalimiana na umati jijini Monrovia, Liberia Aprili, 1978. **PICHA: MTANDAO**

**NA CHRISTINA MWAKANGALE**

KESHO ndiyo mazishi ya rais wa zamani wa Marekani, Jimmy Carter (100), aliyeacha historia ikiwamo kusaka na kupata amani kati ya Misri na Israeli akiweka mafanikio ya juu ya kidiplomasia, Mashariki ya Kati.

Kiongozi huyo alishinda Tuzo ya Amani ya Nobel mwaka 2002.

Maziko yake yatafanyika kesho nyumbani kwake kwenye bustani ambayo ni sehemu ya kituo cha Carter 'Jimmy Carter National Historical Park, huko Georgia, karibu na mahali alipozikwa mkewe Rosalynn Carter, aliyefariki na miaka 77, aliyeaga dunia mwaka 2023.

Ni rais pekee ambaye amestaafu na kufariki dunia akiwa na umri wa miaka 100 nchini humo kulingana na historia ya marais wote waliongoza Marekani.

Kituo cha Carter, kilitangaza kifo chake Desemba 29, 2024, kilichotokea jijini Georgia.

Carter, alikuwa rais wa 39 akiongoza Marekani kutoka kwa Gerald Ford wa Republican mwaka 1976, lakini akashindwa na Donald Regan mwaka 1980, akiwa ameongoza kwa muhula mmoja.

Mmoja wa watoto wake anamsifu akisema: "Baba yangu alikuwa shujaa, si kwangu tu bali kwa kila mtu anayeamini katika amani, haki za binadamu, upendo usio na ubinafsi," anasema Chip Carter.

"Ndugu zangu, dada na mimi tulishiriki naye wote. Dunia ni familia yetu kwa sababu ya jinsi alivyoleta watu pamoja. Tunakushukuru kwa kuendelea kuheshimu kumbukumbu yake."

Anasema kutakuwa na sherehe za umma huko Atlanta na Washington, D.C na kufuatiwa na maziko ya kifamilia huko Plains, Georgia.

Anakumbusha kuwa taasisi yake ya 'The Carter Center' imesaidia kuboresha maisha ya watu katika zaidi ya nchi 80 kwa kutatua migogoro, kuendeleza demokrasia, haki za binadamu na fursa za kiuchumi, kuzuia magonjwa na kuboresha huduma za afya ya akili.

> "Ndugu zangu, dada na mimi tulishiriki naye wote. Dunia ni familia yetu kwa sababu ya jinsi alivyoleta watu pamoja. Tunakushukuru kwa kuendelea kuheshimu kumbukumbu yake."

Kituo hicho kilianzishwa mwaka 1982 na Carter na mkewe Rosalynn Carter, kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Emory, ili kuendeleza amani na afya duniani.

Amehudumu kama rais kuanzia mwaka 1977 hadi 1981, kipindi ambacho kilikumbwa na migogoro ya kiuchumi na kidiplomasia.

Baada ya kuondoka Ikulu ya White House na viwango vya chini vya idhini, sifa yake ilirejeshwa kupitia kazi ya kibinadamu ambayo ilimletea ushindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel.

**JIMMY CARTER**

Carter, ambaye kabla ya kuwa rais alikuwa Gavana wa Georgia, Luteni wa Jeshi la Wanamaji la Marekani na mkulima wa karanga alikuwa rais wa kwanza wa Marekani kufanya ziara ya kiserikali barani Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara na kutangaza kumalizika kwa siku mbaya kwa Marekani.

Kushamiri kwa bara hilo ni mahali ambako urithi wa Carter kuhusu kazi za haki za binadamu bado zinaonekana sana. Marais wa awali walionesha mtazamo hasi na kutokujali Afrika.

Carter alihamasisha demokrasia kote katika bara hilo na alikaribia kufanikisha azma yake ya kuondoa minyoo ya Guinea, tatizo ambalo liliwaathiri mamilioni ya watu wa taifa hilo.

Waziri wa Afya wa Ethiopia anasema: "Rais Carter alifanya kazi kwa ajili ya binadamu wote bila ya kujali rangi, dini au hadhi." Ethiopia ina zaidi ya watu milioni 110, huku mtu mmoja akiripotiwa kuwa na aina ya minyoo ya Guinea mwaka 2023.

Jimmy Carter, aliingia madarakani akiahidi kuwa hata siku moja hatawadanganya watu wa Marekani.

Katika matokeo ya kashfa ya Watergate, mkulima huyo wa zamani wa karanga kutoka jimboni Georgia aliwasamehe waliokwepa rasimu ya Vietnam na kuwa kiongozi wa kwanza wa Marekani kuchukulia kwa uzito mabadiliko ya tabia nchi.

Katika hatua ya kimataifa, alisaidia kupata makubaliano ya kihistoria ya amani kati ya Misri na Israeli, lakini alijitahidi kukabiliana na mzozo wa mateka wa Iran na uvamizi wa Usovieti nchini Afghanistan.

Mwezi Oktoba mwaka jana alisherehekea siku yake ya kuzaliwa ya 100, wakati huo akitibiwa saratani akipata matibabu kwa miezi 19.

Carter alizaliwa Oktoba 1, 1924 katika mji mdogo wa Plains, Georgia, akiwa mkubwa kati ya watoto wanne wa familia yake.

Baba yake alikuwa ameanzisha biashara ya familia ya karanga na mama yake, Lillian, alikuwa muuguzi aliyesajiliwa.

Uzoefu wa Carter na imani thabiti ya Kibaptisti ulitengeneza falsafa yake ya kisiasa.

Mchezaji nyota wa mpira wa vikapu katika shule ya upili, aliendelea kukaa miaka saba katika Jeshi la Wanamaji la Marekani wakati huo alimuoa Rosalynn, rafiki wa dada yake na kuwa ofisa wa manowari.

Lakini baada ya kifo cha baba yake mnamo 1953, alirudi kuendesha shamba la familia.

**KUPIGANIA HAKI**

Wakati siasa za Marekani zikipamba moto kufuatia uamuzi wa Mahakama ya Juu wa kuondoa ubaguzi wa rangi shuleni, Carter alitarajiwa kupinga na kuleta mageuzi.

Wakati akihudumu kwa mihula miwili katika Seneti ya jimbo, aliepuka mizozo na watu wanaobagua, ikiwa ni pamoja na ndani ya Chama cha Democratic.

Lakini alipokuwa Gavana wa Georgia mnamo 1970, alizidi kuunga mkono haki za raia. Alifanya kampeni ya haki za kiraia katika miaka ya 1960.

Anasema:"Nawaambia kwa uwazi kabisa, kwamba wakati wa ubaguzi wa rangi umekwisha."

Aliweka picha za Martin Luther King kwenye kuta za jengo la makao makuu. Alihakikisha kwamba Waamerika wenye asili ya Kiafrika wanateuliwa katika ofisi za umma.

# Joto uchaguzi ndani ya CHADEMA ni makundi timu Mbowe, Lissu

**NA HALFANI CHUSI**

FUKUTO la uchaguzi ndani ya CHADEMA kuwapata mwenyekiti taifa limepamba moto na hata kuibua makundi yanayosigana kuwaunga mkono au kuwapinga wagombea wa nafasi hiyo.

Vigogo hao Tundu Lissu na Freeman Mbowe, wanaitaka nafasi ya uenyekiti wakati wanaogombea nafasi ya makamu ni John Heche na Ezekiel Wenje.

Makundi yanayoonyesha msimamo ni la kumuunga mkono Lissu na jingine la Mbowe, yote yakikwaruzana kwenye majukwaa mitaani na kwenye mitandao ya kijamii. Wakijiita au 'team Lissu' ama 'team Mbowe'

Hata hivyo, pamoja na kuwapo makundi hakuna upande unaorusha kejeli, matusi na kashfa dhidi ya mwingine, zaidi ya kujenga hoja za kuvuta wapiga kura.

Katika moja ya hotuba zake, Lissu ambaye awali anaonyesha kusudio la kutetea nafasi yake ya makamu, kabla ya kubatilisha uamuzi wa kuvaana Mbowe kuwa Mwenyekiti Taifa, anasema:

"Nimejitafakari nimeona kwa sasa ni wakati sahihi wa kuwania nafasi hiyo."

Hata hivyo Lissu aliwahi kusema anania ya kuwania nafasi ya urais kwa awamu nyingine, japo vyanzo vya ndani ya chama hicho vinasema hajakubaliwa.

Hata hivyo, kushindikana kwa mpango huo, kunahusishwa na mpango wa Lissu kuutaka uenyekiti ili aweze kuwa na nafasi ya kuamua kutekeleza hilo.

Katika hotuba zake hivi karibuni Lissu amekuwa akisema mara nyingi iwapo uchaguzi huo hautofanyika kwa haki atakuwa na uamuzi mwingine ambao hakuuweka hadharani.

Udadisi wa gazeti hili kutoka kwa vyanzo ndani ya chama hicho, vinasema iwapo uchaguzi huo utakuwa na makandokando na Lissu akaanguka kwa viashiria visivyo vya haki huenda akajiunga na ACT Wazalendo.

Kutimia kwa hilo, pengine kutampa tena nafasi ya kuwania nafasi ya urais akiwa katika chama hicho kutokana na ukubwa wake na ushawishi wa kisiasa alio nao.

Lissu anaamini kama uchaguzi utafanyika kwa haki atashinda na kuendeleza mazuri yaliyofanywa na Mbowe kwa kipindi chote alichokaa madarakani.

"Kwasababu hiyo wana CHADEMA au mtu mwingine yeyote anayeona ajabu, au anayechukizwa au kukwazwa na uamuzi wangu wakutangaza nia ya kugombea uongozi ndani ya chama chetu atakuwa au amesahau, ama hajui na pengine hataki kuenzi na kue ndeleza urithi tulioachiwa wazee wetu Edwin Mtei na Bob Makani wakuachiana madaraka ya uongozi ndani ya chama kupitia uchaguzi huru na haki."

Anaongeza: "Mtu wa aina hiyo anatakiwa kuelimishwa au kukumbushwa urithi wetu huu na kwa vyovyote vile asiruhusiwe kutuletea utamadani tofauti katika kubadilishana madaraka na uongozi katika chama chetu."




Mgombea wa urais CHADEMA 2020 ,Tundu Lissu , akipoke begi lenye fomu ya kugombea nafasi hiyo kutoka kwa viongozi wa chama . **PICHA: MTANDAO**

Anasema Lissu anapotangaza kuwania uenyekiti.

Kubadili kwake msimamo wa kuwa makamu mwenyekiti tangu alipoanza kushawishiwa kugombea nafasi hiyo mwaka 2015 kunatokana na mazingira ya siasa ya sasa ambayo yanahitaji kiongozi mwenye historia ya uadilifu na kukubalika na jamii, anaongeza.

"Ndugu zangu na wanachama tupo katika mazingira mapya katika siasa za nchi yetu...Hatua hii ya sasa inahitaji kiongozi mwenye historia ya uadilifu na kukubalika na jamii. Ninapenda kuamaini kwamba historia ya kukubalika kwangu kwa Watanzania inajulikana na wengi," anasema.

Aidha, anasema hatua hiyo ya mapambano ya kidemokrasia inahitaji kiongozi aliyeonesha kwa maneno ya katiba kwa tabia na mwenendo wa uzalendo wa kupenda na kutetea nchi.

Kutokana na chama hicho kukua kwasasa hakuna budi kurudisha tena, utaratibu wa kikatiba wa ukomo wa madaraka katika chama hicho uliokuwapo mwanzo.

### MSIMAMO WA MBOWE

Pamoja na kukiongoza chama kwa miongo miwili anasema ametafakari kwa kina jambo hilo na kuamua kutetea nafasi yake, kutokana na maoni kutoka kwa wadau tofauti.

"Nimetafakari kwa kina nimesema mara nyingi nilitamani kuondoka lakini siwezi kuondoka na minyukano ambayo ipo ndani ya chama kwa hiyo CHADEMA nipo, nitakuwapo, nitagombea na mimi na viongozi wenzangu wanaoniunga mkono na wasioniunga mkono naamini tutakutana kwenye mazungumzo tuweke mambo sawa, sijawahi kuzuia watu kugombea, anayetaka tukutane kwenye boksi."

Anasema wazee waasisi hawakuondoka madarakani kwa kuwa walitaka kung'atuka, waliamua kuondoka kwasababu walikuwa wametimiza wajibu wao mkubwa wa kujenga chama imara chenye itikadi na sera madhubuti.

Anakumbusha kuwa Edwin Mtei Mwenyekiti wa kwanza CHADEMA aliondoka akiwa na miaka 68, miaka mitano baadaye Bob Makani Mwenyekiti wa pili, aliondoka akiwa na miaka 67 wote waliondoka si kwasababu ya kushindwa bali baada ya kukamilisha kazi za kuimarisha sera.

"Nilipokea kijiti cha kuongoza Septemba 14, 2004, katika miaka hiyo 20 ni kipindi cha miaka 11 tu ya kwanza ambapo tulifanya kazi kikamilifu ya kujitoa ili kukijenga chama chetu kiwe makini na tukapata mafanikio ya kufanya tuwe chama kikuu cha upinzani Tanzania.

"Tumefanya mambo mengi ikiwamo kubuni vazi maarufu la chama ndiyo kombati na kuongeza thamani ya chama chetu kwa kuvuta wanasiasa makini kutoka vyama vyote na vyuoni hadi tukafananishwa na klabu ya Real Madrid inayovuta wacheza nyota 'mastaa' mbalimbali, tukapata wengi waliokuja kuongeza thamani ya CHADEMA," anakumbusha.

### VITA UMAKAMU

Haijaishia tu kwa wagombea nafasi ya uenyekiti sasa mtifuano upo katika nafasi ya makamu inayowaniwa na Mwenyekiti wa CHADEMA kanda ya Victoria, Ezekiah Wenje na aliyekuwa Mbunge wa Tarime, John Heche.

Hotuba za Wenje zinaonyesha anamuunga mkono Mbowe, anayataja matatizo ambayo atashughulika nayo kuwa ni pamoja na ubovu wa miundombinu, ukosefu wa ajira na kuinua sekta muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi.

Wenje anaiomba serikali kuweka mifumo rafiki ya elimu bunifu kwa wanafunzi ili kukabiliana na changamoto za maisha na kuanzisha mitaala ya kujifunza kwa vitendo.

Aidha, anakumbushia kuweka soko la pamoja katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kusaidia kukuza mzunguko wa biashara na kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kuendelea kutegemea soko la Kariakoo lililopo Dar es Salaam.

Heche anayemuunga mkono Lissu, anasema ana mrengo wa kutaka haki, ukweli na uwazi ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani.

Anasema 'Kambi ya Lissu' wana uhakika wa kuchukua kiti na kuongoza chama hicho na kuwa hawako tayari kuona kinaongozwa na malengo ya watu binafsi kinyume cha madhumuni ya kuanzishwa kwake.

"Chama hiki kimeanzishwa kwa madhumuni maalumu ikiwa ni pamoja na kushinda dola na kuiondoa CCM, kulinda na kutumia rasilimali za nchi kwa manufaa ya Watanzania, kuwapatia huduma bora ikiwa ni pamoja na matibabu, elimu na umiliki wa rasilimali binafsi," Heche anasema.

Anaeleza kuwa watu wengi wamefariki dunia kwa namna tofauti katika kuhakikisha wanapigania maslahi ya chama hicho, hivyo hawako tayari kuona kinaongozwa kwa malengo binafsi.

### UCHAGUZI MKUU

Kuhusu chama hicho kushiriki uchaguzi mkuu mwaka huu, Heche anasema wakipata nafasi hiyo hawatakubali kushiriki bila kuwa na mabadiliko ya Tume Huru ya Uchaguzi (INEC).

"Tutapeleka nguvu ya umma na tuna imani watasimama nasi kama walivyofanya katika mabadiliko mbalimbali kuhakikisha tunashinikiza serikali kufanya mabadiliko INEC kabla ya uchaguzi mkuu na tutasimama katika msimamo wetu kuwa 'no reform no election' ikimaanisha kama hakuna mabadiliko hakuna uchaguzi," anasema Heche.

### KUKICHAFUA CHAMA

Kuhusu madai kwamba Lissu anachafua chama, Heche anaunga mkono kampeni za Lissu kuwasema na kuibua kashfa za baadhi ya watu wanaodaiwa kupokea rushwa ndani ya chama hicho.

"Kuna watu wanachafua viongozi wengine, wanamwita Lissu muongo, si kweli. Lissu ni mkweli na mtu safi. Anachokifanya ni kuwavua nguo wanaovua nguo chama na wala si chama chenyewe. Wananchi wakikwambia wanataka mchicha ukawaletea vitu vingine kwa madai zote ni mboga za majani, hawatakuelewa," anasema Heche.

Anasisitiza kuwa anamheshimu mwenyekiti wa sasa, Freeman Mbowe kama baba yake na mlezi wa kisiasa na kuwa haitatokea kumkosea heshima.

Anasema anao mchango katika demokrasia ya taifa na chama chao lakini kwa sasa Lissu ni kimbunga, Tsunami akimaanisha ni wakati wa Mbowe kukaa pembeni.

# MUHTASARI DIRA 2050 (1)

**Na Mwandishi Wetu**

RASIMU ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 inayoandaliwa na Ofisi ya Rais Tume ya Mipango, imefikia hatua ya kuhakikiwa kuanzia mwishoni mwa mwaka jana.

Dira hiyo imeainisha baadhi ya mambo muhimu yaliyoko ndani ya andiko hilo ambalo ni malengo Tanzania inayojiwekea ili kuyatimiza ifikapo 2050 na kupata maendeleo.

Nipashe inakuletea mambo muhimu yaliyoainishwa ili kujua kile taifa linachotarajia kufanya katika miaka 25 ijayo, lakini kwanza kwa kurejea dira inayomaliza muda wake.

**DIRA INAYOMALIZIKA**

Katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, Tanzania imetekeleza dira ya maendeleo ya taifa 2025, ambayo ililenga kuinua uchumi wa nchi hadi hadhi ya kipato cha kati.

Dira hiyo ilijikita katika kuleta mageuzi kupitia kilimo cha kisasa, viwanda, ujenzi wa miundombinu na maendeleo ya kiteknolojia.

Hadi mwaka 2020 taifa lilifikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya chini, ikiwa na wastani wa mapato kwa kila mtu kufikia Dola za Marekani 1080 ambalo ni ongezeko la dola 180 tangu mwaka 2000.

Viwango vya hali ya maisha viliimarika kwa kiasi kikubwa huku kiwango cha umaskini kikishuka kwa asilimia 36 mwaka 2000 hadi asilimia 26 mwaka 2022. Sekta za afya na elimu ziliimarika zaidi, udumavu wa watoto chini ya miaka mitano ulipungua kutoka asilimia 48 mwaka 2005 hadi asilimia 30 mwaka 2022.

Kwa upande wa vifo vya wazazi vilishuka kutoka 675 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2005 hadi kufikia 104 mwaka 2022.

Aidha, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 112 mwaka 2005 hadi 43 mwaka 2022 katika kila vizazi hai 1,000. Huku uandikishaji wa wanafunzi shule za msingi ukifikia asilimia 100 mwaka 2020 kukiwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na sekondari.

Kwa muhtasari ndiyo mafanikio ya Dira ya 2025, lakini pamoja na juhudi hizo, jitihada zaidi zinahitajika kutokomeza maskini na kujenga uchumi imara na jumuishi, kuelekea mwaka 2050.

Tanzania inadhamiria kufanya mageuzi makubwa ya kimaendeleo ya kijamii na kiuchumi ambayo yatalingana au kuzidi ya nchi za kipato cha kati ngazi ya juu.

Hata hivyo, kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 jitihada zaidi zinahitajika ili kukabiliana na mabadiliko makubwa yatakayotokeza ikiwamo ongezeko la idadi ya watu ambalo linatarajiwa kuongezeka mara dufu hadi kufikia 140, zaidi ya nusu wakiwa wanaishi mijini.

Ongezeko la watu linaathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji na usalama wa chakula, makazi, ajira, elimu na huduma za afya, uwekezaji wa kimkakati katika sekta muhimu kama vile kilimo, madini, utalii, viwanda na tekinolojia utakuwa muhimu ili kukuza uchumi kwa zaidi ya mara nne ili kukidhi mahitaji ya kijamii ya wakati huo.

Wakati huo huo, Tanzania italazimika kukabiliana na mabadiliko kadhaa yanayojitokeza duniani, ikiwamo ongezeko la tofauti za kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi, ukuaji wa miji, tekinolojia zinazoibuka na mivutano ya kisiasa. Hata hivyo fursa za kimaendeleo zinaendelea kujitokeza kama vile za kiteknolojia, mabadiliko kuelekea nishati safi na usawa wa kijinsia unaongezeka.

Kwa kutumia idadi kubwa ya vijana wake, rasilimali asilia, nafasi yake kijiografia hasa kuwa na bahari na miundombinu ya usafirishaji , Tanzania inaweza kuendeleza ustawi wake huku ikichangia malengo ya maendeleo endelevu duniani.

Dira 2050 inaweka maono makubwa kwa mustakabali wa taifa na mikakati ili kufikia maendeleo.

Inajengwa juu ya mafanikio na uzoefu wa utekelezaji wa dira 2025 na kuzingatia mabadiliko mbalimbali duniani. Dira 2050 inalenga kuifanya nchi kuwa yenye nguvu kiuchumi brani Afrika na duniani kwa ujumla.

Italiongoza taifa kuwa nchi yenye nguvu kiuchumi barani Afrika na duaniani pia. Italiongoza taifa kuwa na mustakabali endelevu, unaozingatia usawa wa kijinsia hususan wa wanawake, vijana, na wenye ulemavu na ustawi wa watu wake.



Bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere Rufiji, mkakati wa dira 2025 kuongeza umeme.. **PICHA: MTANDAO**

**MUHTASARI DIRA 2050**

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inafikia ukomo na kufungua ukurasa mpya wa kuanza kutumika kwa nyingine itakayoifikisha Tanzania mwaka 2050. Andiko lake sasa limefikia kwenye hatua za rasimu kuhakikiwa na wadau mbalimbali.

**TAMKO**

Inatamka kuwa inakusudia kuifanya Tanzania kuwa taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea, ikiweka mkazo katika maendeleo ya watu (kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania), kukomesha umaskini wa aina zote na kujenga taifa lenye uchumi imara. Halikadhalika dira inalenga kuwa na uchumi jumuishi, ulioshindani na utakaoboresha maisha ya watu mijini na vijijini.

**MISINGI YA DIRA**

Mosi ni kila Mtanzania awe na jukumu la kudumisha Muungano wa Tanzania na Zanzibar, umoja na mshikamano wa taifa, msingi mwingine ni utu, kila mtu anastahili kuheshimiwa na kuthaminiwa pamoja na kulindwa utu wake.

Msingi wa tatu wa dira hii ni uhuru na haki, kwamba kila raia ana haki ya kufurahia haki zote na uhuru wa kulindwa kwa mujibu wa katiba.

Demokrasia ni msingi mwingine unaosisitizwa, ukieleza kuwa kila mtu, jamii na taifa kuwa na jukumu la kuheshimu, kulinda na kudumisha demokrasia, utawala bora unaofuata sheria na unaoheshimu na kuzingatia katiba.

Ulinzi wa maliasili na rasilimali unatajwa kuwa msingi muhimu wa dira hii unaosisitiza kulinda na matumizi endelevu ya rasilimali za Tanzania kwa ajili ya maendeleo ya watu wake.

> Viwango vya hali ya maisha viliimarika kwa kiasi kikubwa huku kiwango cha umaskini kikishuka kwa asilimia 36 mwaka 2000 hadi asilimia 26 mwaka 2022. Sekta za afya na elimu ziliimarika zaidi, udumavu wa watoto chini ya miaka mitano ulipungua kutoka asilimia 48 mwaka 2005 hadi asilimia 30 mwaka 2022.

"Hivyo, malialisi na rasilimali za taifa zitalindwa, kusimamiwa na kutumiwa vyema kwa maendeleo endelevu na ustawi wa nchi na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo," rasimu ya dira inaeleza.

Ulinzi na utamaduni wa maadili ya taifa ambao ni urithi wa tamaduni wa Watanzania, vitahifadhiwa, kukuzwa na kulindwa ili kujenga utambulisho wa kitaifa na umoja kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**MALENGO YA DIRA**

Dira inalenga kuwa ifikapo 2050 taifa lifikie kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu yenye uchumi, mseto stahimilivu, imara na jumuishi. Aidha, kutokomeza aina zote za umaskini hususan kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu na kuimarisha maendeleo yanayolingana kwa kila mkoa. Kuwa na ubora wa hali ya juu wa maisha na ustawi kwa watu wote.

Kujenga kikamilifu uwezo wa rasilimali watu hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuchochea maendeleo ya taifa na kushiriki kama raia wa kimataifa wenye ubunifu, fikra tunduizi na kujiamini.

Lengo lingine la dira hiyo ni kuwa na mfumo wa utawala ulio jumuishi, wenye uwazi na uhaohakikisha amani ya kudumu, uhuru na usalama wa watu. Aidha, dira pia inalenga kuwa na mfumo imara na endelevu wa usimamizi thabiti na endelevu wa ikolojia na rasilimali ili kujenga ustahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi.

***ITAENDELEA WIKI IJAYO***

## Watakiwa kutunza mazingira, miundombinu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wanaoishi pembezoni mwa barabara ya mzunguko wametakiwa kuwa mabalozi wa kupanda miti ili kulinda mazingira na miundombinu.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Ofisi ya Kilimo,Ufugaji na Utunzaji wa Mazingira, Daimu Mmolosho alitoa wito huo juzi katika Kata ya Msalato Dodoma wakati wa upandaji miti kwenye barabara hiyo.

Mmolosho, aliwaomba wakazi hao kuwa mstari wa mbele kupanda miti na kuhifadhi mazingira na miundombinu iliyopo.

Alisema wamepanda miti hiyo 1,500 kutoka barabara ya Msalato hadi, kwenye mzunguko ili kuitikia wito wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

"Tumepanda miti kuanzia eneo la Msalato kuelekea barabara ya mzunguko eneo la Makutupora kwa ajili ya kutekeleza maelekezo ya Rais kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, tuhakikishe wakazi ambao wanaishi kandokando wanakuwa walinzi na watunzaji wa miti na mazingira," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Msalato, Devotha Selufara, alisema upandaji miti ni kuadhimisha utunzaji mazingira na siku ya usafi wa mazingira bila kuruhusu mifugo kuharibu miche waliyoipanda.

Tukio hilo la upandaji miti liliongozwa na maofisa hao wa Magereza na kushirikisha wananchi, madiwani, watendaji kata, mitaa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

# Maeneo uwekezaji sasa mtandaoni

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Viwanda na Biashara imeiagiza mikoa kuainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji nchini na kuyaweka kwenye tovuti ili kuwarahisishia wawekezaji kuchagua kwa ajili ya biashara zao.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Suleiman Selela, alitoa agizo hilo juzi wakati wa bonanza lililofanyika kwenye Viwanja vya Bombadia Manispaa ya Singida na kuwashirikisha wafanyakazi wa wizara yake na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida.

Dk. Selela, alisema serikali imeboresha mifumo ya biashara ikilinganishwa na miaka ya nyuma wakati ambao mwekezaji wa nje ilikuwa ni lazima aje nchini ndipo apate huduma.

Alisema kwa sasa kupitia serikali mtandao, mwekezaji anaweza kupata taarifa za eneo analotaka kuwekeza akiwa mahali popote.

"Tunasisitiza mikoa maeneo ambayo yanafaa kwa uwekezaji yawekwe kwenye mtandao yaweze kuonekana kwenye mitandao na kwenye tovuti ya mkoa husika ili wawekezaji waone, wizara kazi yetu ni sera, tunachochea mazingira yawe mepesi," alisema.

Selela, alisema pamoja na kwamba changamoto haziwezi kwisha, serikali inataka kama ni changamoto mpya na watu waje wawekeze, viwanda viwepo lije suala la masoko na kujua bidhaa zinazozalishwa zinatumika kwa kiwango gani.

"Hatuhitaji tu kila aina ya kiwanda, tunachohitaji ni aina gani ya kiwanda tunakitaka, viwanda vinavyokuja nchini mtazamo wa Rais na serikali ni kuhakikisha tunapata viwanda ambavyo vinatatua changamoto ya Watanzania," alisema.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema wameuchagua Singida kama wenyeji wa bonanza hilo kutokana na uwepo wake katikati ya nchi, ukuaji wake katika sekta ya viwanda vidogo na vikubwa.

Kigahe, alitoa pongezi kwa uongozi wa mkoa huo kwa maendeleo na mazingira wezeshi ya biashara kwa kampuni na kutenga maeneo bora ya viwanda vidogo na vikubwa

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa huo, Moses Machali, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, alitumia fursa hiyo kuwakaribisha watumishi wa wizara hiyo na wananchi kutembelea Singida kutembelea vivutio mbalimbali vilivyopo.

# Hospitali Mirembe yajengewa maabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya imemshauri Mkandarasi Kiunga Builders kuongeza kasi ya ujenzi wa mradi wa maabara ya kisasa katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ili ukamilike kwa wakati.

Msanifu Majengo wa Wizara hiyo, Seth Akyoo, alitoa ushauri huo juzi baada ya kukagua ujenzi wa mradi huo unaofanywa na chini ya Ufadhili wa Global Fund.

"Nashauri muongeze kasi ya ujenzi ili muweze kukamilisha kwa wakati na nimeona mnaendelea vizuri mpo ndani ya muda kulingana na mpango kazi wa utekelezaji wa mradi huu", alisema Akyoo

Alisema utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo utagharimu kiasi cha Sh. milioni 800 na baada ya kukamilika, utasaidia kuboresha huduma za uchunguzi katika hospitali hiyo.

Msimamizi wa Mradi huo, Mhandisi Jackson Kitundu, alisema wamepokea ushauri huo na kuahidi ujenzi utakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

"Mradi huu ulianza rasmi Desemba 3, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi nane," alisema Kitundu.




Baadhi ya viongozi wa Shirika la Kutetea Haki za Abiria wakiwa katika kikao cha ndani cha kupanga mikakati ya kuimarisha zaidi utendaji kazi wa shirika hilo jijini Dodoma juzi. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima Kongwa kicheko NIRC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKULIMA wa Skimu ya Umwagiliaji Tubugwe Juu iliyopo Wilaya ya Kongwa mkoani hapa, wameishukuru Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) kwa kuichagua kuwa miongoni mwa skimu 23 kunufaika na Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP - P4R).

Shukrani hizo zilitolewa juzi wakati wa mkutano mkuu wa wakulima wa skimu hiyo uliohusisha utiaji saini mkataba wa usimamizi na uendeshaji na matunzo ya skimu.

Mwenyekiti wa skimu hiyo, Zuberi Mwagillo alisema, uwepo wa skimu yao utarejesha matumaini ya wakulima hao kufanya kilimo chenye tija katika maeneo mbalimbali wilayani humo.

Mwagillo, alisema kwa kipindi kirefu wakulima hao walipoteza matumaini ya namna ya kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na maji.

Alisema utiaji saini ya matunzo na usimamizi wa skimu hiyo, utawasaidia wakulima hao kufanya kilimo chenye tija cha mazao ya chakula na biashara.

"Tunaishukuru sana tume kutokana na kuichagua Skimu ya Tubugwe Juu kuwa moja ya itakayonufaika na mradi huo, hii imesaidia kurejesha matumaini ya wakulima wa eneo hili," alisema Mwagillo.

Alisema uharibifu uliopo katika skimu hiyo umechangia kupungua kwa maji kufika katika maeneo yote ya mashamba na kusababisha mazao kukauka na wakulima kushindwa kuendelea na kilimo.

Alifafanua kuwa utekelezaji wa mradi huo katika skimu hiyo, unaohusisha usimamizi, uendeshaji na matunzo ya skimu, utatatua kero hiyo ya muda mrefu na kuwapa matumaini ya kuendelea na kilimo.

Kwa upande mwingine, aliishukuru tume hiyo kwa kuwapatia wakulima elimu ya utekelezaji mradi huo na kutatua changamoto ya usimamizi miundombinu, utunzaji na uendeshaji miundombinu ya umwagiliaji.

Mhandisi wa Umwagiliaji wa Mkoa wa Dodoma, Osward Urassa amewahakikishia wakulima hao watakuwa bega kwa bega kuhakikisha mradi huo unaleta tija na kuongeza uzalishaji.

Tubugwe Juu yenye ukubwa wa ekari 375, inanufaisha wakulima 186 wa vijiji vya Mongwa, Tubugwe Kibaoni na Bumila Wilaya ya Mpwapwa





# Wakulima tumbaku njiapanda

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKULIMA wa Tumbaku wa Kata ya Gua wilayani hapa Mkoa wa Songwe, wameiomba serikali iwaruhusu waendelee kulima mashamba yao yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 500 yanayodaiwa kuwa ndani ya Pori la Akiba la Lukwati ili wasipate hasara.

Wakulima hao wanadai kuwa wamezuiwa kuendelea na maandalizi ya mashamba hayo wakati msimu wa kilimo umefika baada ya kufanya baadhi ya maandalizi na ununuzi wa pembejeo za kilimo.

Baadhi ya wakulima hao wanadai wameshaotesha mbegu kwa ajili ya kupanda na kununua mbolea, lakini Serikali ya Wilaya ya Songwe imewazuia na kuhatarisha uhai wa vyama vyao vya msingi.



Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Wakulima wa Tumbaku cha Gua (Gua AMCOS), Elias Dereva, alisema wakulima wanaoathirika na katazo hilo zaidi ya 80 wa vyama vitatu vya msingi vilivyopo kwenye kata hiyo.

Dereva, alisema baadhi ya wakulima wamelima mashamba yao na kujiandaa kuanza kupanda zao hilo, lakini wanaathiriwa na katazo hilo ambalo al[illegible] limekuja muda ambao sio sahihi.

"Baada ya katazo hili tuliwaita wanachama wetu na kuwaeleza hali ilivyo, wanachoomba ni serikali iwaruhusu washiriki kilimo msimu huu ili waweze kurejesha mikop kwa ajili ya msimu huu," alisema.

Mmoja wa wakulima hao, Bathoromeo Kyando. aliiomba serikali iwaruhusu kuendelea na kilimo kwa msimu huu ili wavinusuru vyama vyao vya ushirika kwa kuwadhamini mikopo ya pembejeo.

Kyando, alisema wanategemea zaidi kilimo cha zao hilo kuendesha uchumi wao, kitendo cha kuwazuia kitasababisha kuzorota.

"Tumelima hapa kwa zaidi ya miaka 10 na huu ulikuwa ni msitu wa kijiji ambao tuliubadilisha matumizi, sasa tumezuiliwa ghafla, tunaomba serikali ituruhusu tuendelee kwa msimu huu," alisema.

Frolah Pima, alimuomba mkuu wa wilaya hiyo kuwasaidia ili waendelee na kilimo na kurejesha mikopo mikubwa kwenye taasisi za fedha na kunusuru mali zao kutaifishwa.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, alithibitisha kuwepo kwa zuio hilo baada ya kuwekwa na Kamati ya Usalama ya Wilaya hiyo kwa lengo la kulinda mazingira.

Itunda, alisema wamepokea malalamiko hayo na maombi yao na kwamba hivi karibuni watafanya kikao kupitia na kuchunguza baadhi ya malalamiko ili maamuzi mapya yatolewe.




Watuhumiwa wa mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kilolo, Christina Nindi Kibiki, wakifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Iringa jana kwa kutajwa kwa mara ya tatu. Kesi imeahirishwa hadi Januari 21, mwaka huu. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Polisi sasa kuwakamata abiria wa bajaj

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limesema abiria wanaozidi kwenye vyombo vya moto hasa bajaji na bodaboda kuwa watachukuliwa hatua kwa kuwashusha na na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga alitangaza kiama hicho juzi kwenye oparesheni ya kukagua makosa mbalimbali ya usalama barabarani.

Kuzaga, alisema bajaji zinatakiwa kubeba abira watatu na abiria ambaye atataka kupanda vyombo hivyo akikuta abiria wamejaa asithubutu kupanda, vinginevyo atachukuliwa hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Alisema wameamua kuanzisha oparesheni hiyo ili kupunguza ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kusababisha madhara kwa binadamu na mali zao.

"Kuna ile tabia ya abiria kwenye bajaji wengine wananing'inia, tukikukuta tutakushusha na kukuchukulia hatua za kisheria, oparesheni hii ni endelevu na mimi mwenyewe nitakuwa nashiriki mara kwa mara," alisema Kuzaga.

Alisema kuna madereva wa pikipiki za abiria wamekuwa wakipakia abiria zaidi ya mmoja maarufu kwa jina la 'mishikaki' hali ambayo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Notca Kilewa aliwataka madereva wa magari ya abiria hasa daladala kuacha tabia ya kukatisha ruti.

Kilewa, alisema kitendo cha kukatisha ruti kinasababisha ongezeko la gharama za maisha kwa wananchi kutokana na kulazimika kulipa nauli mara mbili badala ya moja.

Alisema watakaokamatwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema ajali za barabarani zinapotokea mara nyingi jeshi la polisi ndilo limekuwa likilaumiwa na hivyo wameamua kushughulikia madereva ili kuondoa lawama hizo.

# Wahimizwa kupeleka watoto elimu ya awali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI na walezi wametakiwa kuwapeleka watoto wenye umri kuanzia miaka mitatu hadi mitano elimu ya awali kuwajengea msingi bora wa elimu wakiwa wadogo.

Ofisa Takwimu na Vifaa Divisheni ya Awali na Msingi Benedict Nkumbi, alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa watoto kusoma elimu ya awali wakiwa na umri mdogo katika shule mbalimbali nchini.

Nkumbi, alisema elimu hiyo ina umuhimu kwa watoto wadogo kabla ya kuanza darasa la kwanza kwa kuwa inawasaidia kujifunza vitu mbalimbali ambavyo humjenga ikiwemo kupata nafasi ya kufanya vizuri katika masomo ya msingi.

Alisema elimu hiyo ni bora hasa ukizingatia kwa sasa serikali imewekeza kwa kutoa mafunzo kwa walimu ya namna ya uboreshaji wa kufundisha wanafunzi wa elimu ya awali.

"Naomba wazazi wazingatie umuhimu wa kuwapeleka watoto shule za awali zinawasaidia kupata uelewa kabla ya kujiunga na shule za msingi," alisema Nkumbi.

**Nkumbi, alisema elimu hiyo ina umuhimu kwa watoto wadogo kabla ya kuanza darasa la kwanza kwa kuwa inawasaidia kujifunza vitu mbalimbali ambavyo humjenga ikiwemo kupata nafasi ya kufanya vizuri katika masomo ya msingi.**



## Wakuu wa taasisi wajadili utendaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUKWAA la Wakuu wa Taasisi za Serikali ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Tanzania (SMT) linafanyika visiwani hapa kujadili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Akifungua kongamano la jukwaa hilo jana, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema jukwaa hilo limeweka vipaumbele kuimarisha ushirikiano kuongeza tija, ufanisi, fursa, ujuzi, maarifa, ulezi na ushauri miongoni mwa viongozi wa umma na taasisi.

Alisema jukwaa hilo litaendeleza jitihada za serikali kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kutimiza malengo ya taasisi hizo.

Alitoa rai kwa viongozi wa taasisi za umma na wananchi kutumia jukwaa hilo kujifunza, kubadilishana uzoefu na kutatua changamoto kwenye maeneo yao kwa kuzingatia utawala bora na matumizi sahihi ya rasilimali za umma.

Aliwataka wakuu wa taasisi hizo kuunga mkono jitihada za viongozi wakuu wa nchi na kutekeleza kwa vitendo falsafa ya 4R ya maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kujenga upya Taifa ili kudumisha amani na utulivu.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema lengo la jukwaa hilo ni kutoa fursa kwa wakuu wa taasisi kujadili maono na maelekezo ya viongozi wakuu wa nchi kuwaletea wananchi maendeleo.

Shaaban, alisema jukwaa hilo ni kiungo muhimu na msaada kuhakikisha usimamiaji wa upangaji wa mikakati ya maendeleo na kuzitatua changamoto mbalimbali ili kuboresha huduma katika jamii.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Biashara Tanzania (TANTRED), Latifa Mohamed Khamis, alisema malengo makuu ya jukwaa hilo ni kutoa fursa kwa wajumbe kujifunza na kujengea uzoefu ili kufika malengo ya taifa.

# ZIPA yajivunia kusajili miradi ya mabilioni

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), imesajili miradi ya uwekezaji 430 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.6 kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Hussein Hassan Mwinyi, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Saleh Saad Muhammed, wakati Rais Mwinyi akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Hoteli ya SPD-Buhairan iliyopo Bwejuu Mkoa Kusini Unguja inayomilikiwa na wawekezaji kutoka Falme za Kiarabu.

Muhhamed, alisema pamoja na mafanikio hayo ambayo mamlaka hiyo imepata, miradi hiyo inatarajia kutoa fursa za ajira 25,000 kwa wananchi visiwani hapa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwinyi alisema ongezeko kubwa la wawekezaji katika sekta ya utalii limechangia kukuza uchumi na maendeleo visiwani hapa.

Alisema ongezeko hilo pia linachangia ongezeko la watalii wanaotembelea visiwani hapa na kuimarisha sekta hiyo.

Mwinyi, alisema faida ya utalii ni kubwa kwa nchi katika kukuza uchumi na kuwahimiza wananchi visiwani hapa kuendelea kuwaunga mkono wawekezaji kwenye maeneo yao.

Alizitaja faida hizo kuwa ni fursa za ajira kwa vijana, upatikanaji wa soko kwa bidhaa zinazozalishwa na wakulima na wavuvi kwa bidhaa za baharini na ongezeko la pato la Taifa.

Akizungumzia uwekezaji wa hoteli hiyo, Mwinyi, alisema utafungua milango kwa Zanzibar kupokea wageni wengi zaidi kutoka Falme za Kiarabu.

Kwa upande mwingine, aliridhia ombi lililowasilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud kwa niaba ya wananchi la kutengenezewa barabara ya kilomita tatu kwa kiwango cha lami kutoka Michamvi Mashariki hadi Michamvi Magharibi.

Akizungumza katika hafla hiyo kwa niaba ya mmiliki na mwekezaji wa mradi huo, Dk. Muhammed Omar aliishukuru serikali kwa kukubali kuwekeza kwa manufaa ya wakazi eneo hilo kwa kutoa ajira 500 na kuchangia uchumi wa nchi.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, akikata utepe, kuashiria ufunguzi wa ghala la kuhifadhia nafaka huko Ole Dodeani Wilaya ya Chakechake, ikiwa ni miongoni mwa Shamrashamra za kutimiza Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: PIGAPICHA WETU**

# Serikali yajenga maghala ya chakula

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita amesema serikali imejenga miundombinu ya kuhifadhi mazao ya chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini.

Mwita aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa ghala la kuhifadhia nafaka linalojengwa Ole Dodeani Wilaya ya Chake Chake Pemba, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ujenzi wa majengo hayo, utasaidia kuimarisha biashara ya mazao ya nafaka na kuwa katika hali ya usalama wa chakula.

Mwita, alisema kutokana na matatizo yanayoweza kujitokeza kwa kula chakula kisicho salama, serikali imelipa kipaumbele suala la usalama wa chakula kwa kujenga ghala hilo na mengine visiwani hapa.

Alisema ghala hilo litasaidia kukuza biashara ya utalii kwa wageni wanaoingia nchini kwa kuwa na imani ya kula chakula salama.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Rashid Hadid Rashid, alisifu jitihada za Rais Hussein Mwinyi kwa kuwaunganisha wananchi visiwani hapa katika kilimo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Ali Khamis Juma, alisema mradi huo utasaidia kudhibiti magonjwa yatokanayo na sumu kuvu hasa kwa mazao ya nafaka.

Juma, alisema wizara hiyo inaendelea kuimarisha miundombinu, ujenzi wa maghala mapya na kukarabati makongwe kutokana na kuchakaa.

Ghala hilo limejengwa na Serikali kupitia mradi wa kuhifadhi sumu kuvu Tanzania kuanzia mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu.

Mradi huo umefadhiliwa na Programu ya uhakika wa chakula na lishe chini ya Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo Afrika (ADB).

# Gambo aja na hoja zake kumjibu Makonda

**Na Maulid Mmbaga**

MBUNGE wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, amemjibu Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kuwa yeye si mfanyakazi wa serikali bali ni mwakilishi wa wananchi aliyechaguliwa kwa mujibu wa katiba.

Amesema vikao vinavyotambulika kisheria kwa wabunge ni vile vya Bunge na kamati zake na si jukumu la mkuu wa mkoa kutoa maelekezo juu ya ushiriki wake kwenye vikao vingine.

Gambo alitoa kauli hiyo jana kupitia kipande cha video, akimjibu Makonda ambaye alimshutumu kwa kutohudhuria vikao vinavyojadili maendeleo ya mkoa huo, jambo lililosababisha kutokuwa na taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara.

Sakata hilo liliibuka juzi mkoani Arusha wakati Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, alipokuwa akikagua barabara ya Mianzini - Ngaramtoni. Katika ziara hiyo, Gambo alihoji na kutaka ufafanuzi kutoka kwa Waziri Ulega kwa nini hadi sasa ujenzi wa barabara hizo haujafanyika licha ya mkataba wa ujenzi kutiwa saini tangu mwaka 2023.

Makonda alisema Gambo hahudhurii kwenye vikao na kwamba anasubiri viongozi wa kitaifa ndipo achomekee maneno aliyoyaita kuwa ni ya uchonganishi.

"Utaratibu wa kufanya kazi kwa mujibu wa katiba, sheria na kanuni uko wazi. Mtu anayeweza kutoa taarifa ya kutohudhuria vikao vyangu ni Bunge, si mkuu wa mkoa. Mimi kama mbunge ni wajibu wangu kuwasemea wananchi changamoto zao, si kazi ya kunong'onezana shida za watu," alisema Gambo.

Gambo pia alisisitiza kuwa anawajibika kwa kueleza mafanikio yaliyopatikana na kuikumbusha serikali kuhusu changamoto zinazohitaji kushughulikiwa na kwamba kauli na uelewa wa Makonda kuhusu nafasi ya mbunge na wajibu wake zinahitaji kufafanuliwa.



Paul Makonda



Mrisho Gambo

"Mimi si mtu wa kupokea amri kwa sababu ninatokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM). Wajibu wangu ni kuwasemea wananchi changamoto zao kwa uwazi, siyo kunong'ona. Tunaposhirikiana na viongozi wa kitaifa ni kwa sababu hiyo ndiyo njia ya kufikisha sauti za wananchi," alisema.

Kuhusu hoja alizoziwasilisha Gambo, alisema Juni 16, 2023 walialikwa kushuhudia utiwaji wa saini mkataba wa mradi ambao ungejenga barabara ya Arusha - Kibaya hadi Kongwa yenye urefu wa kilometa 453.4, ambao wangenufaika nao kwa ujenzi kuanzia kona ya Mbauda hadi Bondeni City.

"Ujenzi huo ungesaidia kuondoa msongamano na mafuriko kwa sababu wananchi wa Kata ya Sombetini na maeneo mengine wamekuwa wanateseka kwa muda mrefu. Sasa tulisaini mkataba tangu 2023 lakini mpaka leo (jana) 2025 mkandarasi hayuko saiti.

"Waziri wa Ujenzi ndiye mwenye dhamana kwa hiyo nilitumia fursa hiyo kumwomba atoe ufafanuzi kwa wananchi wajue serikali imejipangaje kutekeleza mradi huo ambao mkataba wake ulisainiwa hadharani na ukiangalia leo ni mwaka 2025 ni kipindi kirefu. Tunahitaji kupata majibu kama wananchi," alisema Gambo.

**ZITTO AINGILIA KATI**

Katika hatua nyingine, Kiongozi Mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, kupitia ukurasa wake wa X, alisema vikao vya Kamati ya Fedha na Mipango ya Manispaa, Baraza la Madiwani na Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC) ni vikao vya kisheria, hivyo utetezi wa Gambo wa kutohudhuria vikao hivyo hauna mashiko.

"Lakini Mrisho, vikao hivyo ni vya kisheria. Wabunge wengi haswa wa siku hizi mnadharau sana vikao vya chini na matokeo yake hamfanyi kazi ya uwakilishi vizuri, huu utetezi wako sio," alisema.

Zitto pia alijibu hoja ya mdau wa mtandao huo aliyeandika wabunge wengi wanajisahau kutokana na kupita bila kupingwa maana wanaamini chama dola kitawabeba na laiti kungekuwa na ushindani wa kweli kwenye sanduku la kura wasingekuwa wazembe.

Zitto akijibu hoja hiyo, aliandika kuwa: "Siyo kujisahau, wabunge wengi wanadharau vikao vya chini. Nilipokuwa mbunge moja ya vikao nilikuwa nahakikisha sikosi ni RCC. Hiki ni kikao ambacho kinakupa sura ya maendeleo ya mkoa mzima. Kuna nyakati kikao kizima nilikuwa mbunge pekee yangu kati ya wabunge wanane wa mkoa."

# COPRA, wataalam kushirikiana kilimo cha kuinua uchumi

**Na Mwandishi Wetu, KAGERA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), imeahidi kushirikiana na wataalam wa kilimo ngazi ya vijiji hadi mkoa kutoa huduma kwa wakulima na wafanyabiashara wa mazao nchini ili kuinua uchumi wao na kuboresha maisha yao.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Irene Mlola, katika ziara Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na kufanya mazungumzo na Katibu Tawala wa mkoa huo, Stephen Ndaki.

Mlola, alisema COPRA imeweka mikakati ya kushirikiana na mikoa na mamlaka za serikali za mitaa nchini ili kuhakikisha wananchi wananufaika na mavuno ya mazao ya nafaka na mchanganyiko na kujikwamua kiuchumi.

"COPRA imejipanga vizuri kuhakikisha wakulima na wafanyabiashara wa mazao wananufaika na mikakati walioiweka. Tunaomba ofisi za mikoa mtoe ushirikiano," alisema Mlola.

Alisema COPRA imeanzisha ofisi za kanda ikiwamo ya Kanda ya Ziwa ili kurahisisha huduma kwa wananchi na wadau walio kwenye mnyororo wa thamani wa mazao mbalimbali nchini.

Alisisitiza kuwa maofisa wa COPRA wataendelea kushirikiana na wataalamu wa kilimo kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa kuwahudumia wananchi ili kuhakikisha wananufaika na sekta ya kilimo.

Vilevile, aliwataka wakulima na wafanyabiashara wa mazao nchini kuchangamkia fursa ya uwapo wa COPRA na kutoa ushirikiano kwa maofisa hao.

Alisema COPRA imejipanga kufanyakazi kwa ushirikiano na watalaam wa kilimo kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa ili wakulima na wafanyabiashara wanufaike na mamlaka hiyo.

Alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa COPRA na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha malengo ya serikali ya kuwawezesha wakulima na wafanyabiashara wa mazao kiuchumi yanatimia.

"Tutaendelea kutoa ushirikiano kwa COPRA lengo letu ni kuona mikakati iliowekwa na serikali kuwainua wakulima na wafanyabiashara nchini inatimia," alisema Ndaki.

Alisema mkoa uko pamoja na mamlaka hiyo kutoa ushirikiaono kwa maofisa wake kuwahudumia wakulima.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TITO ELISANTE KINGU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 239 BXN** aina ya **TOYOTA SPRINTER.** Chassis namba **AE1100121544.** Engine namba **5AG982220.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/1025/2025.**

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 2073/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU TWALIBU JUMA MSANGI WA UBUNGO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABDALLAH JUMA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 mwezi 01 mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 30 mwezi 12 mwaka 2024.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONIFACE JIVAVA SANGA,** anatangaza kupotea kwa Kadi ya Gari ya Ruwaichi Paulo Mambali yenye namba za usajili **T.623 AEJ,** yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi **PHQ/MBE/361/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**JUMIYE KUTA JUMIYE** Anatangaza kupotelewa kwa kadi za bajaji **(TVS KING),** zenye namba za usajili **MC 603 CDA, MC 619 CDF, MC 758 CEB, MC 776 CFF, MC 504 CPF, MC 783 CSJ, MC 264 CVD, MC 329 CVW na MC 311 CWM.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye. **PHQ/MOR/MOR/701/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NURU ELIUD KAPANGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 187 DRQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/884/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**PENDO JULIUS MASELE** Anatangaza kupotelewa kwa kadi za pikipiki **(SINORAY 2)** zenye namba za usajili **MC 701 DWA, na MC 170 DWH.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye. **PHQ/MOR/MOR/39363/2024**

HABARIKIMATAIFA

# Congress yathibitisha ushindi wa Trump

**NEW YORK, Marekani**

MAKAMU wa Rais wa Marekani na aliyekuwa mgombea urais kwa tiketi ya Democratic, Kamala Harris, ameongoza shughuli ya bunge la nchi hiyo kuidhinisha ushindi wa mpinzani wake, Donald Trump, kuwa rais mpya.

Kinyume na hali ilivyokuwa miaka minne iliyopita, siku ya Jumatatu (Januari 6) bunge la Marekani lilifanikisha kwa wepesi tukio hilo ambalo ni alama ya mila ya kidemokrasia kwa taifa hilo kubwa duniani bila ya mashaka yoyote.

Ilielezwa kuwa makamu wa Rais Kamala Harris alisimamia zoezi hilo la kuhe sabiwa kura za wajumbe na kisha akamtangaza rasmi aliyekuwa mpinzani wake kwenye uchaguzi wa Novemba 9 kuwa ndiye mshindi halali.

"Matokeo ya kura ya rais wa Marekani, kama yalivyowasilishwa kwa rais wa Baraza la Seneti ni kama ifuatavyo. Idadi kamili ya wajumbe walioteuliwa kumchagua rais wa Marekani ni 538. Ndani yake, wingi wa kura ni 270. Kura za rais ni kama ifuatavyo: Donald Trump wa jimbo la Florida amepata kura 312. Kamala Harris wa jimbo la Carlifornia amepata kura 226.

"Kura za makamu wa rais ni Vance wa jimbo la Ohio amepata kura 312, Tim Walz wa jimbo la Minnesota amepata kura 226," alisema Harris.

Ilielezwa kuwa kabla ya kutoa tangazo hilo, Kamala Harris alikuwa ametekeleza wajibu wake huo wa kikatiba kwa kusimama kwenye ukumbi wa bunge akipitisha kila nakala ya matokeo ya uchaguzi kwa wabunge na kila karatasi ya matokeo ya kura ilipotajwa alisimama akiwa amekunja mikono yake.

Pia ilielezwa kuwa makamu huyo wa rais kutokea chama cha Democrat alisema kuwa kwake ilikuwa siku muhimu sana kwa demokrasia ya Marekani, akisema "hii ndiyo mila Wamarekani wanayopaswa kuifurahia, ambayo ni mojawapo ya misingi muhimu ya demokrasia yetu".

"Ni muhimu kufanya ukabidhianaji wa madaraka kwa njia za amani. Na leo 'jana' nimetenda kile ambacho nimekuwa nikikifanya maishani mwangu , ambacho ni kutimiza kiapo changu cha kuilinda katiba ya Marekani," alisema Harris.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa kwa hatua hiyo Harris alikuwa anajiunga na orodha ya watangulizi wake ambao walisimamia shughuli ya kuthibitisha kushindwa kwao kwenye uchaguzi kama sehemu ya majukumu yao ya kikatiba kwenye bunge.

Richard Nixon alifanya vivyo hivyo pale aliposhindwa na John Kennedy mwaka 1960 na akafuatiwa na mgombea urais kwa tiketi ya Democrat mwaka 2000, Al Gor, pale Mahakama ya Juu ya Katiba iliporidhia kuchaguliwa kwa George Bush.

Januari 6, 2021, wafuasi wa Trump, aliyekuwa wakati huo ameshindwa kwenye uchaguzi wa rais na Joe Biden, walilivamia jengo la Capitol Hill, na kusababisha madhara makubwa yakiwemo vifo, katika jaribio la kulizuwia bunge kumuidhinisha rasmi Joe Biden.

Inaelezwa kuwa hadi sasa, watuhumiwa wa machafuko hayo wanaendelea kushikiliwa jela, na wengi wanatazamia watatangaziwa msamaha mara tu Trump atakapoapishwa wiki mbili zijazo.

***DW***



Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, akisimamia uthibitishwaji wa ushindi wa Donald Trump kuwa rais wa Marekani bungeni, jana. **PICHA: MTANDAO.**

## UN: Watu milioni 30 wanahitaji msaada Sudani

**KHARTOUM, Sudan**

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema zaidi ya watu milioni 30 nchini Sudan, nusu wakiwa ni watoto wana uhitaji wa dharura wa misaada ya kibinadamu, baada ya maisha yao kutatizwa kutokana na vita vinavyoendelea kati ya jeshi na wanamgambo wa Kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na UN, ili kuwasaidia watu hao, Dola Bilioni 4.2 (Sh. Trilioni 10.3) zinahitaji kutoka kwa wahisani, ili kuwafikia raia wa nchi hiyo zaidi ya milioni 30.

Pia umoja huo ulisema kati ya watu hao, milioni 20.9 wapo katika hali mbaya sana na wanahitaji msaada wa haraka kama chakula, maji safi, makazi na dawa huku dunia ikionywa kuwa imeisahau Sudan na macho yote kuangazia Ukraine na vita vya Mashariki ya Kati.

Wito huu unakuja, baada ya hali ya ukame kutangazwa katika majimbo matano ya Sudan na hivyo kusababisha watu wengine zaidi ya milioni nane kuwa katika hatari ya kukabiliwa na njaa kali.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa vita nchini Sudani vilivyoanza Aprili mwaka 2023 kati ya majenerali wawili wanaotaka kuongoza nchi hiyo, vimesababisha vifo vya maelfu ya watu, huku wengine zaidi ya milioni 2.7 wakiyahama makazi yao.

Vile vile, ilibainishwa kuwa watu wengine zaidi ya milioni 3.3 wamevuka mpaka na kwenda kutafuta hifadhi katika mataifa jirani kama Chad na Sudani Kusini.

***RFI***

## Macron: Afrika ilisahau kuishukuru Ufaransa

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron amesema kuwa mataifa ya Afrika yalisahau kuishukuru Ufaransa kwa kunusuru mataifa yao kuwa chini ya udhibiti wa wanamgambo, huku akisema hilo litafanyika kwa wakati.

Maoni ya kiongozi huyo yalitolewa jana wakati wa mkutano wa kila mwaka huko jijini Paris kwa mabalozi wa Ufaransa na ulizingatia malengo ya sera ya kigeni ya Ufaransa kwa mwaka 2025.

"Nadhani walisahau kutushukuru, lakini ni sawa, itakuja kwa wakati. Hakuna hata mmoja wao angelikuwa na serikali huru kama Ufaransa isingepeleka jeshi lake katika eneo hilo," alisema Rais Macron.

Tovuti ya habari ya Alwhida Info ilichapisha kwamba, Waziri wa Mambo ya Nje wa Chad, Abderaman Koulamallah alimjibu kiongozi huyo akisema "Afrika, ikiwemo Chad, iliisaidia Ufaransa kwa kiwango kikubwa wakati wa vita viwili vya dunia, jambo ambalo Ufaransa haijawahi kukubali".

Pia Koulamallah alisema viongozi wa Ufaransa wanastahili kuheshimu watu wa Afrika na kutambua thamani ya kujitolea kwao.

Waziri Mkuu wa Senegal Ousmane Sonko alipuuza jukumu la Ufaransa katika kuhakikisha nchi za Afrika zina uhuru, akiishutumu Paris kwa kufanya kinyume na hilo.

"Macron anajigamba kwamba hakuna nchi ya Kiafrika ambayo leo ingekuwa huru kama haingesaidiwa na Ufaransa," Sonko aliandika kwenye mtandao wake wa Facebook.

"Tutambue kwamba Ufaransa haina uwezo wala uhalali wa kuyahakikishia usalama mataifa ya Afrika," aliongeza, akiituhumu kwa kuchangia machafuko ya Libya na kuilaumu kwa kuchochea hali tete ya usalama katika eneo la Sahel.

Sonko alisema tangazo la Novemba 2024 kwamba Ufaransa itafunga kambi zake za kijeshi nchini Senegal lilitokana na juhudi za taifa hilo la Kiafrika kama nchi huru, inayojitawala.

***BBC***

# Sabato atua rasmi Prisons

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mkongwe kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Kelvin Sabato 'Kiduku', amejiunga na Klabu ya Prisons, akitokea Fountain Gate, katika kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa Prisons imemsajili kwa mkataba wa miezi sita ambayo ina kipengele cha kumwongezea mkataba mwishoni mwa msimu kama ataonesha kiwango bora.

Pamoja na kwamba Prisons haijathibitisha hilo, lakini tayari picha za mchezaji huyo akisaini kwa maafande hao zimevuja, huku mtoa taarifa akisema kwa sasa wanaweka mambo sawa wakisubiri siku rasmi ya kumtambulisha.

"Tunaendelea kufanya maboresho ya kikosi chetu baada ya kuonekana kuwa na mapungufu makubwa kwenye mzunguko wa kwanza, hatupo sehemu nzuri na lengo letu namba moja kwa sasa ni kubaki Ligi Kuu," kilisema chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo.

Unakuwa ni usajili wa kwanza kwa timu hiyo, ambayo imeahidi kuongeza baadhi ya wachezaji kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao

Sabato ambaye mashabiki wake wanamwita 'Kiduku', ni mmoja kati ya wachezaji waliozichezea timu nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Baadhi ya timu alizozichezea ni Mtibwa Sugar, Singida Big Stars, Polisi Tanzania, Namungo, Singida Black Stars na Fountain Gate.

Atakuwa na kazi kubwa ya kufanya, kwani Prisons ipo nafasi ya 13 ya msimamo wa ligi hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, ikikusanya pointi 14 katika michezo 16 iliyocheza, ikishinda mitatu, sare tano na imepoteza mechi nane.

Tayari klabu hiyo imeshampa mkono wa kwa heri kocha wao, Mbwana Makata kwa kile ilichodai kutokuwa na matokeo mazuri katika michezo ya mzunguko wa kwanza, huku kocha wa Geita Gold, Amani Josiah, akitarajia kuchukua nafasi yake.

# KOCHA MPYA SINGIDA AANZA KAZI, ATAKA MALENGO KUFIKIWA

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu mpya wa Singida Black Stars, Hamdi Miloud, juzi ametembelea kambi ya timu hiyo na jana alitarajiwa kuanza kazi rasmi ya kuinoa timu hiyo baada ya kutangazwa hivi karibuni, huku akisema anataka wachezaji wenye ari na wapambanaji na si vinginevyo.

Akizungumza na wachezaji wa timu hiyo alipowatembelea kambini, Singida, kocha huyo alisema pamoja na kipaji cha mchezaji alichonacho, lakini peke yake hakitoshi kama hatokuwa na njaa, ari na upambanaji katika kikosi chake ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Ninafuraha kubwa kuwa hapa nanyi pamoja, nimekuja na msaidizi wangu kuona tunapata matokeo bora kwa kila mmoja wenu kucheza kwa ari na kupambana," alisema kocha huyo mwenye uraia pacha wa Algeria na Ufaransa."

Alisema alikuwa na mikutano kadhaa na viongozi wa klabu hiyo na amefurahia malengo yao, hivyo atakapoanza kazi, ataanzia pale ambapo wengine wameishia.

"Kuanzia kesho (jana), nitakuwa kambini kuelezea ni namna gani tunapaswa kufanya kazi kuanzia mazoezi, malengo, na kila kitu tutakachotekeleza pamoja, tunatakiwa kufanya kazi kwa kujitoa na bidii, ili tuweze kufanya kitu kikubwa sana tukiwa kama timu.

"Ninataka kuyaendelea malengo yetu hatua kwa hatua, tukitoa juhudi zetu zote na kila kitu kitaanzia kwenye mazoezi ya kwanza, hivyo kazi inaanza, na nina imani kwamba kwa pamoja tutafanikisha malengo yetu, ahsanteni sana, nawatakia mwanzo mwema wa safari hii yenye mafanikio mbele yetu," alisema.

Kocha huyo amechukua nafasi ya Mbelgiji Patrick Aussems, ambaye alioneshwa mlango wa kutokea Novemba mwaka jana, nafasi yake ikachukuliwa na Mkurugenzi wa Ufundi wa Klabu hiyo, Ramadhani Nsanzurwimo, ambaye kwa sasa amerejea kwenye majukumu yake ya awali.

Rekodi zinaonesha kuwa kocha huyo amezifundisha Klabu za USM Alger na JS Kabylie za Algeria, Al- Salmiya ya Kuwait, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Athletico Marseille na ES Vitrolles za Ufaransa na Al- Ettifaq FC ya Saudia Arabia.

Katika historia yake ya soka, amefanikiwa kufika robo fainali tatu za michuano ya kimataifa, Afrika, akifanya hivyo dhidi ya JS Kablie mara mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na USM Alger katika Kombe la Shirikisho la Soka Afrika.

**UMETUHESHIMISHA...**




Luka Modric (katikati), akipongezwa na wachezaji wenzake wa Real Madrid, baada ya kuifungia timu yao bao la tano wakati wakishinda 5-0 dhidi ya Deportiva Minera kwenye mechi ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey) iliyopigwa Uwanja wa Estadio Cartagonova juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Tanesco, Nyumbu, vinara 'First League'

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Nyumbu FC ya Pwani na Tanesco ya Kilimanjaro, zinaongoza kwenye First League (Ligi Daraja la Pili) inayoendelea kusaka timu zitakazopanda Championship (Ligi Daraja la Kwanza), kwa msimu ujao.

Wakati Nyumbu, ikiliongoza Kundi A, Tanesco ni kinara wa Kundi B, huku kila timu kwenye makundi yote mawili ikicheza michezo sita.

Msimamo wa Kundi A, wenye timu nane, unaonesha kuwa Nyumbu FC inaongozwa ikiwa na pointi 11, ikiwa imecheza michezo sita, ikishinda mitatu, sare mbili na kupoteza mchezo mmoja.

Timu hiyo inafuatiwa na Hausung FC, yenye pointi tisa, Pan African nafasi ya tatu na pointi zake nane, Tunduru Korosho ipo nafasi ya nne pia ikiwa na pointi nane, huku Magnet FC ikishika nafasi ya tano kwa kukusanya pointi saba.

Nafasi ya sita ipo Dar City ikiwa na pointi sita, Moro Kids ya saba na pointi zake tano, African Lyon inaburuza mkia, ikiwa na pointi mbili tu, haijashinda hata mchezo mmoja, ikipoteza minne na sare mbili.

Kundi B, ambalo pia lina timu nane linaongozwa na Tanesco FC, ambayo imejikusanyia pointi 14, ikishinda nne na sare mbili, Rhino Rangers nafasi ya pili ikiwa na pointi 13, na Mapinduzi FC ina pointi kumi ikiwa nafasi ya tatu.

Timu ya TRA inakamata nafasi ya nne ikiwa na pointi tisa, Gunners FC ya tano ikikusanya pointi nane, Copco FC ya sita na pointi zake tano, Alliance FC ya saba, huku Ruvu Shooting ikishika mkia ikiambulia pointi moja tu, katika michezo sita iliyocheza.

## ZISIKUPITE

### DURAN ATAKIWA PSG

PARIS St-Germain ina nia ya kumsajili Jhon Duran na inaaminika Aston Villa inaweza kushawishika kumuuza mshambuliaji huyo wa Colombia mwenye umri wa miaka 21 kwa pauni milioni 60. ***(Sportsport)***

### BARCA NAO WAMTAKA

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco, amekutana na wawakilishi wa Jhon Duran kwa mazungumzo yasiyo rasmi ili kumjulisha mshambuliaji huyo wa Aston Villa kuwa yuko kwenye rada za klabu hiyo ya Katalunya. ***(Sport)***

### GYOKERES AWANIWA BAYERN

BAYERN Munich inataka kuvuruga ombi la Manchester United la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26, kutoka Sporting. ***(Star)***

### VAN DIJK AKATALIWA MADRID

REAL Madrid imekataa nafasi ya kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 33, ambaye atakuwa mchezaji huru mkataba wake na Liverpool utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(Relevo)***

### CASEMIRO ASUBIRIWA SAUDIA

LIGI Kuu ya Saudia Arabia ina matumaini ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 32, kutoka Manchester United mwezi huu. ***(Telegraph)***

### MUANI KWA MKOPO

MANCHESTER United na Tottenham Hotspur zinatathimini uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Randal Kolo Muani kwa mkopo kutoka Paris St-Germain, huku Juventus pia ikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Athletic)***

### RASHFORD ATAKIWA MILAN

MARCUS Rashford mwenye umri wa miaka 27, anasakwa kwa mkopo na AC Milan, lakini mkataba wowote utategemea Manchester United kulipa sehemu kubwa ya mshahara wa mshambuliaji huyo wa England. ***(Guardian)***

### ZIRKZEE HAITAKI JUVENTUS

JUVENTUS ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee kwa mkopo, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hana nia ya kuondoka Manchester United. ***(Sky Sports)***

### VLAHOVIC KUBADILISHWA

KLABU ya Manchester United imepewa ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 24, katika mkataba wa kubadilishana na Joshua Zirkzee. ***(Team Talk)***

### REAL BETIS KWA ANTONY

REAL Betis ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazotarajia kumsajili winga wa Manchester United na Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, kwa mkopo kwa msimu uliosalia. ***(Independent)***

### FULLKRUG ANATAKIWA JUVE

MSHAMBULIAJI wa West Ham, Niclas Fullkrug, pia ananyatiwa na Juventus, huku klabu hiyo ya Italia ikitaka kumsajili kwa mkopo mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 31. ***(Calciomercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# OLMO, VICTOR WAMZULIA BALAA LAPORTA BARCA

●●● Sasa atakiwa kujiuzulu urais wa klabu hiyo kutokana na kushindwa kukamilisha...

**BARCELONA, Hispania**

MAKUNDI ya mashabiki mbalimbali yamemtaka rais wa Barcelona, Joan Laporta, kujiuzulu kutokana na kushindwa kuwasajili Dani Olmo na Pau Victor.

Vyama 10 tofauti na vikundi vya mashabiki wa klabu hiyo, vikiongozwa na kundi la Si al Futur, Victor Font na Joan Camprubi Montal wa Som un Clam wamekutana kumtaka Laporta ajiuzulu.

Wanataja „uzembe" katika kumsajili Olmo na Victor na sasa wanamtaka kujiuzulu kwa raia huyo ambaye anatakiwa kuwa madarakani hadi 2026.

Taarifa iliyotiwa saini na makundi hayo 10 ilieleza kama Laporta hatajiuzulu, watafikiria kuongeza kura ya kutokuwa na imani dhidi yake.

LaLiga na Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), lilitangaza Jumamosi kwamba Barca haiwezi kuwasajili tena Olmo na Victor kwa mara ya pili msimu huu kutokana na mgogoro wa kifedha wa klabu hiyo kuthibitishwa kuwa hauwezi kuzingatia usawa wa fedha wa ligi (Sheria za FFP).

Barca wametangaza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa mahakama ya juu zaidi ya michezo nchini humo.

Vyanzo vya klabu vinaendelea kuamini kuwa hatimaye watakuwa na Olmo na Victor tena msimu huu, huku wachezaji wote wawili wakiwa wametajwa kwenye kikosi kwa ajili ya kusafiri kwa ndege hadi Saudi Arabia wiki hii kwa mchezo wa Supercopa ya Hispania.

Barca wataomba kwanza „hatua ya tahadhari" kuwekwa ambayo itawaruhusu wote wawili kucheza ikisubiri uamuzi wa mwisho katika kesi hiyo.

Olmo na Victor walikuwa wamepewa usajili wa muda tu na LaLiga huku Barça wakitumia fursa ya sheria iliyowaruhusu kutumia asilimia 80 ya mshahara kutokana na mchezaji aliyeumia kwa muda mrefu, Andreas. Christensen - kusajili mbadala.

Wachezaji wote wawili wana vifungu katika mikataba yao ambavyo vitawaruhusu kuondoka bila malipo ikiwa hawatasajiliwa kwa kipindi cha pili cha msimu.

# Guardiola ampa onyo Grealish

**MANCHESTER, England**



KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amekiri kuwa Jack Grealish lazima aimarishe kiwango chake cha uchezaji kama anataka kurejesha nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Grealish, aliyesajiliwa kwa pauni milioni 100 mwaka 2021, alishindwa kufunga bao hata moja la klabu mwaka 2024 na hivi karibuni amepoteza nafasi yake kwenye kikosi cha City baada ya Savinho kuwasili majira ya kiangazi.

Alipoulizwa kwa nini Savinho alikuwa akicheza mbele ya Grealish, Guardiola alitoa tu onyo kwa Mwingereza huyo.

"Ni rahisi," alisema Guardiola.

„Kwa jinsi anavyojitazama, ataona ushindani na kwamba lazima ashindane, yeye mwenyewe. Savinho yuko katika hali nzuri na kila kitu kuliko Jack na ndio maana ninamchezesha Savinho.

"Ninataka kiwango cha Jack aliyeshinda mataji matatu? Ndiyo, nataka. Lakini ninajaribu kuwa mkweli kwangu kwa hilo.

"Unaweza kusema si haki. Ikiwa unafikiri hivyo, basi ni sawa. Lakini unapaswa kuthibitisha na kusema, ‚sawa, nitapigana na Savinho, ili kustahili kucheza katika nafasi hiyo kila siku, kila wiki na kila mwezi'.

"Nilimpigania sana Grealish, nilipigania sana kuwa hapa, na najua kuwa anaweza kurejesha kiwango. Nimeona kiwango chake na ninataka kila kipindi cha mazoezi na kila mchezo mmoja, kuna Savinho.

"Je, kuna mtu katika chumba hiki ambaye anadhani Savinho hastahili kucheza hivi sasa? Hapana, anastahili kucheza. Ndiyo maana ninamchezesha - kwa sababu anatoa kila kinachohitajika.

"Ndiyo sababu anacheza. Sina shaka yoyote kuhusu ubora wa Jack au mchezaji yeyote kati ya hawa, vinginevyo wasingekuwa hapa."

# Pulisic, Abraham waipa Milan Super Cup

**MILAN, Italia**

BAO la dakika za nyongeza kutoka kwa Tammy Abraham liliifanya AC Milan kutoka nyuma na kushinda taji la Super Cup la Italia kwa ushindi mnono wa mabao 3-2 dhidi ya wapinzani wao wa jijini moja, Inter Milan katika mchezo wa fainali Jumatatu mjini Riyadh.

Nyota wa Marekani, Christian Pulisic, alifunga bao la kusawazisha kwa Milan kuwa sawa na wapinzani wao kwenye uwanja wa Al-Awwal Park, na kisha akacheza pasi muhimu kuifungua ngome ya Inter kwenye bao la ushindi lililofungwa na Abraham.

Ushindi huo uliinyima Inter kile ambacho kingekuwa taji la nne mfululizo la Super Cup, na kuruhusu Milan kuifikia Inter kwa kutwaa taji hilo mara nane, huku kocha mpya Serge Conceicao akinyanyua kombe katika mchezo wake wa pili akiwa kocha.

"Timu ina tabia, iliweza kushinda mechi dhidi ya timu mbili kubwa mwishoni," alisema Conceicao akiiambia Mediaset.

„Wakati wa mapumziko kocha lazima abadilishe baadhi ya mambo, ndiyo maana wananilipa."



# VAN DIJK NA REAL MADRID

**LIVERPOOL, England**

MAWAKILI wa beki wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk, wameripotiwa walifanya mazungumzo na Real Madrid ili Mholanzi huyo asajiliwe katika klabu hiyo kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake ukikaribia kumalizika hapo Anfield.

Sasa katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake, Van Dijk ni mmoja wa wachezaji watatu wenye hadhi ya juu wanaosababisha wasiwasi mkubwa kwa Liverpool huku mikataba yao ikifikia mwisho.

Mohamed Salah anaendelea kuweka shinikizo kubwa la kutaka kuondoka, huku beki wa kulia Trent Alexander-Arnold ndiye anayelengwa zaidi na Real Madrid kwenye dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

Kwa mujibu wa Relevo, Madrid pia walipewa nafasi ya kumnasa Van Dijk.

Mawakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, wanasemekana walifika ili kujadili uhamisho mkubwa wa bure, wakijua Madrid wanataka kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Van Dijk alipoulizwa hadharani kuhusu uhamisho wa kwenda Madrid, alipuuza uvumi huo haraka.

Sasa, Liverpool wanaaminika kuwa wanajiamini kuhusu nafasi yao ya kupata mustakabali wa Van Dijk kwa mkataba mpya, lakini mashaka yamesalia kuhusu Alexander-Arnold baada ya Madrid kujaribu kuharakisha mipango yao kwa kutaka kumnunua raia huyo wa England Januari hii.

# MPEPO KUREJEA LIGI KUU BARA

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Tanzania Prisons na Geita Gold, Eliuter Mpepo, huenda akaonekana tena kwenye mikikimikiki ya Ligi Kuu Bara baada ya klabu mbili kuingia vitani kusaka saini yake.

Mpepo ambaye alikuwa akicheza Ligi Kuu ya Zambia, inaelezwa yupo kwenye mazungumzo na Klabu ya Tabora United huku pia Kengold FC nao wakitajwa kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Taarifa kutoka ndani ya Klabu ya Tabora United zinaeleza kuwa mazungumzo yao na Mpepo yanaenda vizuri na huenda wakamtangaza kuwa mchezaji wao kabla ya dirisha dogo kufungwa.

"Bado hatujafikia muafaka, lakini tupo kwenye mazungumzo kuangalia uwezekano wa kumsajili ya kukiongezea nguvu kikosi chetu kwa ajili ya mzunguko wa pili," alisema mmoja wa viongozi wa klabu hiyo.

Kiongozi huyo alisema Mpepo wameona ni mchezaji muafaka wa kuongeza nguvu kwenye safu yao ya ushambuliaji kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Mbali na Tabora United, nyota huyo pia anawaniwa na Kengold na Tanzania Prisons aliyoichezea huko nyuma na kutoa mchango mkubwa.

Mpepo alijiunga na Klabu ya Trident akitokea Mtibwa Sugar msimu wa 2023/2024, lakini kwa sasa nyota huyo ameachana na timu hiyo.

NIMEMALIZAAA...




Mshambuliaji wa AC Milan, Tammy Abraham, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la ushindi wakati ikishinda 3-2 dhidi ya Inter Milan, kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Italia (Italian Super Cup), iliyopigwa Uwanja wa Kingdom Arena, Riyadh, Saudi Arabia, usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MTANDAO**

# Okutu akataa kwa mkopo KenGold

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA Erick Okutu wa Pamba Jiji, amekataa mpango wa kupelekwa KenGold kwa mkopo akisema ni bora avunje mkataba wake wa miezi sita uliobaki kuliko kupelekwa timu asiyoitaka.

Okutu, raia wa Ghana, amesema hayo kutokana na tetesi kuwa atatolewa kwa mkopo kwenye Klabu ya KenGold katika kipindi chake cha mkataba uliobaki.

Alisema hana taarifa yoyote ya kwenda KenGold, akisema yeye anafahamu kuwa ni mchezaji halali wa Pamba Jiji.

„Sina taarifa juu ya kutolewa kwa mkopo kwani ninachofahamu bado nina mkataba wa miezi sita na kikosi hiki, sina mpango wowote wa kuondoka, labda itokee ofa kutoka nje ya nchi," alisema.

Imeelezwa kuwa viongozi wa Pamba wanahitaji kumpeleka Okutu kwa mkopo KenGold baada ya kumsajili mshambuliaji raia wa Mkenya, Mathew Tegisi Momanyi, kutoka Shabana FC ya nchi humo.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Pamba, Ezekiel Ntibikeha, alisema masuala ya usajili na kila kitu kinachoendelea kitawekwa hadharani muda utakapowadia na sasa wanachofanya ni kazi ya kuboresha kikosi.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema sababu za nyota huyo kutaka kutolewa ni kutokana na kukorofishana na kocha wa timu hiyo, Fred Felix 'Minziro', alipojibizana naye kutokana na kuoneshwa kadi nyekundu katika mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Prisons Desemba 26, mwaka jana.

Nyota huyo alijiunga na timu hiyo msimu huu baada ya kuachana na Tabora United aliyojiunga nayo mara ya kwanza msimu wa 2023.24, akitoka Hearts of Lions ya Ghana. Msimu uliopita alipachika mabao saba kwenye Ligi Kuu.

## Yanga na hesabu kali kuivaa Al Hilal

INATOKA UK. 24

chohitaji zaidi ya ushindi, tukipata pointi tatu basi tutakuwa na matumaini kwa sababu mechi yetu ya mwisho dhidi ya MC Alger tutacheza tukiwa nyumbani," alisema Kamwe.

Kamwe, pia aliwapa habari nzuri kwa wanachama na mashabiki wa Yanga kwa urejeo wa mchezaji Clatous Chama ambaye kwa muda mrefu hakuwa uwanjani kutokana na kukabiliwa na majeraha.

"Wachezaji wako vizuri na Chama amepona, amerejea kwenye kikosi na atakuwa mmoja kati ya watakaosafiri, ila Yao Kouassi ndiyo bado majeruhi, hatakuwapo kwenye kikosi," alisema.

Yanga ambayo ilipoteza mechi zake mbili za kwanza, kwa mabao 2-0 dhidi ya Al Hilal na MC Alger, lakini ilikuja kuzinduka na kuzoa pointi zote nne kwa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ambapo ilipata sare ya bao 1-1 ugenini na kuifunga mabao 3-1 nchini.

Kwa sasa ipo nafasi ya tatu ya masimamo wa Kundi A, ikiwa na pointi nne, hivyo inahitaji ushindi kwenye mchezo wa Jumapili ili kufikisha pointi saba.

Yanga inakwenda kucheza na timu ambayo tayari imeshafuzu hatua ya robo fainali ikifikisha pointi 10, lakini wenyeji bado wanahitaji ushindi ili kumaliza kinara wa kundi kwa ajili ya kupata faida mbele ya safari kwa kucheza na mshindi wa pili wa makundi mengine, pia kuanzia ugenini mechi za robo fainali na kumalizia nyumbani.

## Simba yatamba kurudia rekodi

INATOKA UK. 24

hesabu kubwa sana, mchezo ujao ni kwa ajili ya kutinga robo fainali na wa mwisho dhidi ya CS Constantine ya Algeria ni maalum kwa kutaka kuongoza kundi," alisema.

Kocha Mkuu, Fadlu Davids, alisema ushindi walioupata Jumapili nchini Tunisia haukuwa rahisi kwani walicheza na moja ya timu kubwa barani Afrika, lakini pia uwanja haukuwa mzuri.

"CS Sfaxien ni moja kati ya timu kubwa barani Afrika, ina uzoefu, kwa hiyo haukuwa ushindi uliopatikana kirahisi, uwanja pia haukuwa mzuri sana, lakini kikubwa ni matokeo.

"Kwa sasa tunahitaji sare ili tufuzu, ingawa hatutacheza ili kusaka sare, bali ushindi na mechi ya mwisho tutataka tushinde ili tuongoze kundi, lakini haraka iwezekanavyo tunataka kufuzu kwenda robo, tutafanya kila linalowezekana lengo litimie," alisema Fadlu.

Simba ilirejea usiku wa kumkia jana ikitokea nchini Tunisia ambako ilifunga CS Sfaxien bao 1-0 lililowekwa ndani ya nyavu na Jean Ahoua na kuifanya kufikisha pointi tisa, ikiwa nafasi ya pili ya msimamo wa Kundi A.

# Michezo

Jumatano Januari 8, 2025

Nipashe


**Olmo, Victor wamzulia balaa Laporta Barca**

UKURASA 21





**MWALI...**



Nahodha wa AC Milan, Davide Calabria, akinyanyua juu Kombe la Italia (Italian Super Cup), baada ya timu hiyo kulitwaa usiku wa kuamkia jana kwa kuichapa Inter Milan mabao 3-2, kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Kingdom Arena, Riyadh, Saudi Arabia. **HABARI UK. 22. PICHA: MTANDAO**

# Yanga na hesabu kali kuivaa Al Hilal

●●●Yaeleza yalipo makali yao huku ikipanga kucheza kwa tahadhari, Chama arejea huku...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kinatarajia kuondoka saa 10:00 alfajiri ya kuamkia kesho kuelekea nchini Mauritania kwa ajili ya mchezo wa raundi ya tano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan.

Mchezo huo unatarajiwa kuchezwa nchini Mauritania Jumapili ijayo saa 4:00 usiku kwenye Uwanja wa De la Capitale, jijini Nouakchott, huku Yanga itashuka dimbani katika mechi hiyo kwa tahadhari kubwa, ikitangaza pia urejeo wa kiungo mshambuliaji wao, Clatous Chama.

Al Hilal inacheza mechi zake nchini humo kutokana na kuwapo kwa machafuko ya kisiasa nchini Sudan.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema inabidi waende nchini huko kwa tahadhari na kucheza mechi kwa mahesabu makubwa kutokana na ugumu na umuhimu wa mchezo huo ambao kwao hauhitaji chochote zaidi ya ushindi.

"Tunakwenda huko kwa ajili ya kusaka pointi tatu tu na si vinginevyo, tutakwenda kucheza kwa tahadhari kubwa kulingana na ubora wa mpinzani wetu, hatutakwenda kufunguka sana kwa sababu Al Hilal ni timu yenye ubora zaidi linapokuja suala la mashambulizi ya kushtukiza, ni mechi ngumu ambayo inabidi twende kucheza kwa mahesabu makali kwani hatuna tuna-

INAENDELEA UK. 23

## Simba yatamba kurudia rekodi ya 1993 Angola

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema Jumapili ijayo inataka kurudia ilichokifanya mwaka 1993, ilipofanikiwa kufuzu fainali ya Kombe la CAF, ambalo sasa linaitwa Kombe la Shirikisho barani Afrika, ikiwa nchini Angola, dhidi ya Atletico Spotivo Aviacao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema haitokuwa mara ya kwanza kushinda au kufuzu ikiwa nchini humo, kwani ilishawahi kushinda mwaka 2022 ikicheza na Primeiro de Agosto mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na ilifuzu mwaka 1993 ilipocheza dhidi ya Atletico Spotivo Aviacao.

"Safari hii tunataka kuingia robo fainali tukiwa ugenini, tunafahamu ugumu wa Bravo do Maquis hasa akiwa nyumbani kwake, lakini tumejipanga vizuri kwenda kupata matokeo Angola na hii haitakiwa mara ya kwanza kushinda au kufuzu, tumeshaenda kucheza pale na Primeiro de Agosto ambao ni wakubwa kuliko Bravo, na tumeshawahi kufuzu hapo hapo Angola dhidi ya Atletico Spotivo Aviacao mwaka 1993 kwenye Kombe la CAF," alisema Ahmed.

Historia inaonesha kuwa Simba ilifuzu hatua ya fainali ya Kombe la CAF ikiwa nchini Angola mwaka 1993, ilipolazimisha suluhu dhidi ya Atletico Spotivo Aviacao, ambapo ulikuwa ni mchezo wa marudiano baada ya ule wa kwanza kushinda mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), jijini Dar es Salaam.

Pia Simba ilishinda mchezo wake nchini Angola kwa mabao 3-1 dhidi ya Primeiro de Agosto, Oktoba 9, 2022, ikiwa ni raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, na katika mchezo ya marudiano uliochezwa nchini, Oktoba 16, 2022, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ilishinda bao 1-0, na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi.

"Kama si kesho Jumatano, basi Alhamisi tutaondoka kuelekea kwenye mchezo wetu muhimu, michezo hii miwili iliyobakia inachezwa kwa

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >